


ZIWA NGOSI



HOSPITALI YA KANDA MBEYA



JIJI LA MBEYA



MPUNGA

# UHURU
*ya kijani*

ISSN 0876 - 3896 Na. 0036
Alhamisi Desemba 7, 2023

**Hii ndiyo Mbeya na fursa tele za uwekezaji**

# TOLEO MAALUM MAFANIKIO MKOA WA MBEYA



MHE. DK. SAMIA SULUHU HASSAN
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



JUMA ZUBERI HOMERA - MKUU WA MKOA WA MBEYA



RODRICK LAZARO MPOGOLO - KATIBU TAWALA MKOA WA MBEYA





Mnara wa Mashujaa Mbeya Mjini


Jengo Jipya la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mbeya

# ZIJUE FURSA 18 ZA UWEKEZAJI NDANI YA MKOA WA MBEYA

**Na KOKU DAVID-**
*MBEYA.*

## 1. HISTORIA YA MKOA WA MBEYA

Mkoa wa Mbeya upo kusini magharibi upande wa nyanda za juu kusini mwa Tanzania. Mkoa upo kati ya latitude 70 and 90 31' kusini mwa Equator na kati ya longitude 320 na 350 Mashariki mwa Greenwich.

Mwaka 2015, Mkoa wa Mbeya uligawanyika katika Mikoa miwili ya Mbeya na Songwe. Makao Makuu ya Mkoa yapo karibu na Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Mkoa wa Mbeya unapakana na Nchi ya Malawi na Mkoa wa Songwe upande wa magharibi, Mkoa wa Singida na Tabora upande wa Kaskazini na Mkoa wa Iringa na Njombe upande wa Mashariki na eneo la Kasumulu katika Wilaya ya Kyela ikiwa ni lango kuu la kuingilia na kutoka katika nchi jirani ya Malawi..

Mkoa wa Mbeya mwanzo ulikuwa unaitwa Mkoa wa Jimbo la nyanda za juu kusini. Mwaka 1963, Jimbo la Nyanda za Juu Kusini liligawanyika katika Mikoa miwili ambayo ni Mkoa wa Mbeya na Iringa.

Mwaka 1972, Mkoa wa Mbeya uliongezewa kipande cha Wilaya ya Sumbawanga ambacho kabla ya hapo kilikuwa katika jimbo la Magharibi. Hata hivyo, kipande cha Wilaya ya Sumbawanga hakikuchukua muda mrefu katika Mkoa wa Mbeya kwani mwaka 1974 Wilaya ya Sumbawanga ulitengwa na kupata hadhi ya kuitwa Mkoa.

## UTANGULIZI

### 2. Eneo, Idadi ya Watu.

Mkoa wa Mbeya una eneo la kilometa za mraba 35,960 zilizogawanyika katika Wilaya 5 na Halmashauri 7. Wilaya zimegawanyika katika Tarafa 15, Kata 179, Vijiji 533 na Mitaa 181.

Kwa Mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 Mkoa wa Mbeya umekuwa na watu 2,343,754 na kati yao Wanawake ni 1,219,926 na Wanaume ni 1,123,828. Wastani wa ongezeko la idadi ya watu ni 3.2%.

### 3. Pato la Mkoa.

Uchumi wa Mkoa unategemea kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, uvunaji mazao ya maliasili, biashara, uzalishaji viwandani na ajira katika Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi.

Pato la Mkoa limekuwa likiongezeka kila mwaka ambapo mwaka 2015 lilikuwa Tshs. trilioni 5.3037, mwaka 2016 Tshs. trilioni 6.0914, mwaka 2017 Tshs. trilioni 6.6632, mwaka 2018 Tshs. trilioni 7.2962, mwaka 2019 Tshs. trilioni 7.8499, mwaka 2020 Tshs. trilioni 8.3521 na mwaka 2021 limefikia Tshs. trilioni 9.0834.

Kwa upande wa pato la Mtu mmoja mmoja pia limekuwa likiongezeka kutoka Tshs. milioni 2,882,915 mwaka 2015 hadi kufikia Tshs. milioni 3,994,044 mwaka 2021.

Katika uchangiaji wa Pato la Taifa, Mkoa kwa mwaka 2021 ulichangia asilimia 5.62 na kufanikiwa kushika nafasi ya tatu.


Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Rufaa Meta

### 4. Fursa za Uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Mbeya.

Julai, 2023 Mkoa ulitenga jumla ya ekari 79,280.369 kwa ajili ya uwekezaji wa Viwanda katika Halmashauri zote. Mkoa unaendelea kuhamasisha Halmashauri za Wilaya kutenga maeneo mengi zaidi pamoja na kuyajengea miundombinu yote muhimu ili yaweze kuuzika kwa Wawekezaji wa ndani na nje ya Mkoa.

Fursa za Uwekezaji zilizopo zimegawanyika katika maeneo mbalimbali kama vile;

Uchimbaji wa Madini Wilaya ya Chunya.

Kilimo cha parachichi Wilaya ya Rungwe na Mbeya

Kilimo cha zao la Mpunga wilaya ya Mbarali na Kyela

Kilimo cha zao la kakao Wilaya ya Kyela na Rungwe

Kilimo cha zao la tumbaku wilaya ya Chunya

Kilimo cha pareto wilaya ya Mbeya

Kilimo cha kahawa wilaya ya Mbeya na Rungwe

Kilimo cha alizeti katika Wilaya ya Chunya na Mbarali

Uwepo wa reli ya TAZARA ni fursa ya usafirishaji wa mizigo kwenda nchi za jirani

Uwepo wa uwanja wa ndege wa Songwe ni fursa kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa mbalimbali na mazao ya kilimo

Uwepo wa bandari ya Itungi (Itungi Port) husaidia usafirishaji wa mizigo kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa biashara.

Uwepo wa hali ya hewa nzuri na mvua za kutosha ni fursa kwa ajili ya kuwekeza katika kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

Uwepo wa misitu, maliasili na utalii ni fursa kwa ajili ya uwekezaji

Uwepo wa ziwa nyasa ni fursa kwa ajili ya uvuvi wa samaki

Fursa za uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji

Fursa za ufugaji wa mifugo mbalimbali Uwepo wa gesi asilia katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

Uwepo wa vyanzo vingi vya utalii Wilaya ya Rungwe na Kyela.

### 5. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 hadi 2022/2023.

#### 5.1. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SEKRETARIETI YA MKOA

#### 5.2.1. Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya

Mradi wa ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya unatekelezwa kwa mfumo wa Force Account. Mradi huu umegawanyika sehemu kuu mbili, moja ni ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambao utekelezaji wake ulianza Juni 11, 2020 na kukamilika mwaka Disemba, 2022.

Awamu ya pili ilikua ni kujenga landscape na kazi za nje ya jengo ambao utekelezaji wake ulianza mwezi Mei, 2022 na ulitarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023. Jengo kuu lina ukubwa wa mita za mraba 5,457. Ujenzi wa ofisi hii umegharimu jumla ya Tshs. bil. 7,715,696,445.00 na unahusisha ujenzi wa Jengo kuu (Main Building), eneo la maegesho ya magari, Bustani, mgahawa wa chakula, Wigo na Ofisi za Walinzi.

Utekelezaji wa mradi wa Jengo jipya la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa umefikia asilimia 99.5, ujenzi wa landscape na kazi za nje ya jengo nao umefikia asilimia 90 na kwamba jengo kuu limeshaanza kutumika, hivi sasa kazi zinazoendelea ni kukamilisha ufungaji wa lift mashine na kazi ndogondogo (snag list and pending works).

Mradi umelenga kuboresha Usalama na Mazingira ya utendaji kazi wa watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwani jengo lililokuwepo awali lilijengwa mwaka 1930 na Serikali ya Kikoloni kwa matofali ya udongo ambapo mpaka mwezi Januari 2020 Ofisi ya mkuu wa Mkoa ilikuwa ikitumia majengo ya zamani.

Serikali ya awamu ya Sita imefanikiwa kujenga nyumba mpya 2 za Makatibu Tawala wa Wilaya za Chunya na Rungwe pamoja na Ofisi 3 za Maafisa Tarafa katika Tarafa za Tukuyu - Rungwe na Tarafa za Unyakyusa na Ntebela wilayani Kyela.



Ramani ya Mkoa wa Mbeya na Wilaya zake

## 6. MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZA KATIKA HALMASHAURI

### SEKTA YA ELIMU

#### 6.1 Elimu ya Awali

Mkoa wa Mbeya una madarasa ya awali 825 kati yake 766 yapo katika shule za Serikali na 59 katika shule zisizo za Serikali.

Mwaka 2023 tulitegemea kuandikisha wanafunzi wa awali 55,997 (Wavulana 27,449 na Wasichana 28,548) ambapo hadi Machi 31, 2023 tuliandikisha Wanafunzi 61,274 (Wavulana 31,057 na Wasichana 30,217) ambao ni sawa na asilimia 109.42. Miongoni mwao wanafunzi 221 (wavulana 147, wasichana 74) ni wenye mahitaji maalumu.

#### 6.2. Elimu ya Msingi (Darasa la I – VII)

Mkoa una shule za msingi 825 zikiwemo shule 766 za Serikali na 59 zisizo za Serikali. Shule hizi zina jumla ya Wanafunzi 413,610 (Wav. 205,083 na Was. 208,527) wa Darasa I – VII.

Kwa mwaka 2023 tulitegemea kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza 61,437 (wavulana 30,749 na wasichana 30,688) ambapo hadi Machi 31 tumeandikisha Wanafunzi 66,545 (wavulana 33,384 na wasichana 33,364) ambao ni sawa na asilimia 108.3. Kati ya hao, wanafunzi 101(wavulana 64, wasichana 37) ni wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Ufaulu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi umepanda kutoka 67.6% mwaka 2017 hadi kufikia 89.22% mwaka 2022

#### 6.4. Elimu Sekondari.

Mpaka sasa Mkoa una jumla ya shule za sekondari 276, kati yake 203 ni za serikali na 73 ni za watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Kati ya shule hizi 61 zina kidato cha tano na sita, 25 zikimilikiwa na serikali na 36 zisizo za serikali.

Shule hizi zina jumla ya wanafunzi 145,876. Aidha wanafunzi waliopangwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za Mkoa wa Mbeya ni 45,666 (wavulana 21,472 na wasichana 24,194) kati ya hao mpaka Machi 31, 2023 walioripoti ni 43,725 sawa na asilimia 95.75.

Ufaulu wa watahiniwa wa kidato cha nne (CSEE) tangu mwaka 2017 umekuwa na mafanikio makubwa ya kutoka 81.4% mwaka 2017 hadi 90.09% mwaka 2022 na kwa upande wa kidato cha sita mwaka 2023 ufaulu ulikuwa asilimia 99.92.

#### 6.6. Miradi ya Ujenzi Sekta ya Elimu.

Kwa mwaka wa Fedha,




# ZIJUE FURSA 18 ZA UWEKEZAJI NDANI YA MKOA WA MBEYA

2021/22, Mkoa wa Mbeya ulipokea jumla ya Tshs. bil. 29,026,622,148 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu. Kati ya fedha hizo Tshs. bil. 19,277,383,972 ni kwa ajili ya miradi ya shule za sekondari, Tshs. bil. 5,378,000,000 ni miradi ya shule za awali na msingi huku Tshs. bil. 4,371,238,176 zikiwa za miradi ya vyuo vikuu na vyuo vya VETA.

Kwa mwaka 2022/2023, Mkoa wa Mbeya ulipokea kiasi cha Tshs. bil. 22,745,693,528.00 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika sekta ya Elimu. Miradi iliyotekelezwa kutokana na fedha hizo ni pamoja na ujenzi wa shule mpya za msingi na sekondari, vyumba vya madarasa, mabweni, matundu ya vyoo na maabara. Fedha hizo ziliíetwa kupitia program za SEQUIP, EP4R, BARRICK, BOOST, GPE LANES na Fedha kutoka Serikali Kuu.

### SHULE YA MKOA YA WASICHANA.

Mkoa ulipokea kiasi cha Tshs. milioni 3,000,000,000 Mei 31, 2023 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Mkoa ya Wasichana itakayojengwa Kyela Kata ya Busale.

Mradi wa BARRICK.

Kupitia ufadhili ya BARRICK, Mkoa ulitengewa Tshs. milioni 399,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa 5, mabweni 2 na matundu 7 ya vyoo katika shule za sekondari ya Iduda na Tukuyu (Rungwe). Miradi hiyo imekamilika.


Fedha Kutoka Serikali Kuu- Ujenzi wa Upanuzi wa Miundombinu ya Kidato cha Tano na ukamilishaji wa miundombinu.

Mkoa ulipokea Tshs. bil. 1,038,000,000.00 Mei 23, 2023 kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya kidato cha tano na sita. Fedha zilitoka serikali kuu ambapo zilielekezwa kujenga mabweni 5, madarasa 11 na matundu ya vyoo 16 katika sekondari za Iwalanje (Mbeya DC), Loleza na Rungwe (Rungwe).

Aidha, Aprili 25, 2023 tulipokea jumla ya Tshs. milioni 390,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya shule za sekondari za Busokelo Girls na Lwangwa (Busokelo), Iwalanje, Galijembe, Inyala, Ilembo, Utengule Usongwe, Ijombe na Nsalala (Mbeya DC) ambapo yalijengwa mabweni 2, mabwalo 6, na maabara 2 na ujenzi huu umekamilika.



Ujenzi wa nyumba ya Katibu Tawala Wilaya ya Chunya



Mradi wa ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita laki 1 katika Mradi wa Maji Ruduga – Mawindi kijiji cha Ipwani Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.



Zao la kokoa Kyela DC



Zao la kahawa Rungwe DC

### MRADI WA BOOST

Mkoa ulipokea ya Tshs. bil. 8,120,200,000.00 Aprili 22, 2023 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 11 na ujenzi wa baadhi ya vyumba vya madarasa na vyoo katika shule 40 ambapo ujenzi wake umekamilika.

### MRADI YA GPE-LANES

Mkoa ulipokea jumla ya Tshs. milioni 766,233,332.00 Machi 7, 2023 kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya GPE-LANES kwa ujenzi wa madarasa ya awali ya mfano, mabweni ya wenye mahitaji maalumu pamoja na ukarabati wa vituo wa vituo vya TRC na ujenzi wake umeshakamilika.

Mradi wa Ujenzi wa Madarasa kupitia Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Jamii na Mapambano dhidi ya Ugonjwa wa UVIKO 19.

Mkoa wa Mbeya kwa mwaka wa fedha 2021/2012, ulipokea fedha Tshs. bil. 12.88 kutoka Serikali Kuu kupitia Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Jamii na Mapambano dhidi ya Ugonjwa wa UVIKO 19 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 464 katika shule za Sekondari, na vyumba 172 vya madarasa kwa shule za msingi katika vituo shikizi.

### 6.7. Vyuo vya Kati na Elimu ya Juu

Mkoa wa Mbeya una vyuo vya Ualimu 05 vikiwemo 02 vya Serikali na 03 visivyo vya Serikali, vyuo vikuu 3 ikiwa ni pamoja na matawi 4 ya vyuo vikuu.

## 7. SEKTA YA AFYA, LISHE NA USTAWI WA JAMII.

Mkoa una jumla ya vituo vya tiba 395 ikijumuisha hospitali 20, vituo vya afya 42 na zahanati 333. Kati ya vituo hivyo vilivyopo, vituo 289 vinamilikiwa na serikali na vituo 106 vinamilikiwa na taasisi/watu binafsi.

### 7.1. Ujenzi wa Vituo vya Afya na Zahanati.

Mkoa wa Mbeya kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ulipokea jumla ya TShs. bil. 11,800,000,000 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo 14 vya afya katika awamu tano.

### 7.2. Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali za Wilaya

Mkoa unaendelea na ujenzi wa Hospitali mpya 3 katika Halmashauri za Mbarali, Mbeya na Busokelo ambapo jumla ya Tshs bil. 4.5 zilipokelewa kwa mwaka wa fedha 2018/19. Hospitali hizi zilianza na majengo saba ya awali ambayo yamekamilika na kuanza kutoa baadhi ya huduma.

Aidha mwaka wa fedha 2019/20 Mkoa ulitengewa kiasi cha Tshs. bil. 2 ili kuendelea na ujenzi wa Hospitali hizo pamoja na kuanza ujenzi wa Hospitali mpya katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Katika hatua nyingine, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilipokea Tshs. milioni 400,000,000 kutoka Global Fund kwa ajili ya ukarabati wa hospitali ya Wilaya ya Rungwe na ujenzi wa jengo la Afya ya Uzazi na Mtoto ambalo limekamilika na linatumika.

Katika mwaka 2020/21 hospitali za Wilaya za Mbarali, Mbeya DC na Busokelo zilitengewa kiasi cha Tshs. bil. 1,500,000,000 wastani wa Tshs. milioni 500,000,000 kila mmoja kwa ajili ya ujenzi wa wodi 3. Wodi hizi zilijengwa na kukamilika.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela pia ilipokea Tshs. milioni 500,000,000 kwa ajili ya Ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto katika hospitali ya Wilaya na ujenzi unaendelea umefikia asilimia 78.

### 7.4. Ujenzi wa Wodi ya Wazazi Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya

Utekelezaji wa mradi huu umeweka historia katika Mkoa Mbeya kwani tangu kuanza kwa hospitali ya Rufaa haijawahi kuongezewa jengo kwa ajili ya kulaza wagonjwa hali iliyokuwa ikisababisha msongamano uliopelekea baadhi ya wagonjwa kulala chini. Ujenzi wa wodi hiyo ya wazazi yenye kuweza kubeba vitanda 222 vya kulaza wagonjwa umegharimu Tshs. bil. 12,329,277,541.99 na kwamba imekuwa mkombozi katika Mkoa wa Mbeya kutokana na kuwa wanawake huweza kujifungua bila wasiwasi.

Jengo hili ambalo liliwekewa Jiwe la Msingi Agosti, 2022 na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari limepokea vifaa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya huduma za afya ya uzazi na mtoto vyenye thamani Tshs. bil. 5,423,319,500.00 na kuufanya mradi huo wote kugharimu Tshs. bil. 17,752,597,041.99.

### 7.5. MASHINE YA MRI (MAGNETIC RESONANCE IMAGING)

Hospitali imepokea mashine ya MRI kutoka Wizara ya Afya kupitia mradi wa ORIO na imegharimu Tshs. bil. 2,678,000,000. Mashine hiyo imeshaanza kufanya kazi tangu Julai 11, 2023 na wagonjwa 28 wamefanyiwa kipimo hicho.

7.6. Miradi ya Afya kwa Fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19.

Mkoa wa Mbeya ulipokea Tshs. bil. 1,690,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa majengo 3 ya huduma za dharura (Chunya DC, Mbarali DC na Rungwe DC), Jengo 1 la Wagonjwa mahututi (ICU) katika Halmashauri ya Mbeya DC, Nyumba 6 za Watumishi kwenye Hospitali za Halmashauri (Busokelo, Kyela, Chunya, Mbarali, Mbeya DC na Rungwe).

Pia Mkoa ulipokea mashine za Mionzi kwa Hospitali 3 ambazo ni Mbarali DC, Mbeya DC na Mbeya Jiji zenye thamani ya Tshs. bil. 1,260,000,000 .

7.7. Ujenzi wa Vituo vya Afya Kwenye Tarafa zisizo na Vituo vya Afya kwa Fedha za Tozo za Miamala.

Katika Kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Juni 2022 Mkoa ulipokea Tshs. bil. 4,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 8 katika Tarafa zisizo na vituo vya afya kwenye Halmashauri zote saba za Mkoa wa Mbeya ambavyo ni Njisi na Itunge(Kyela DC), Itagano(Mbeya Jiji), Swaya(Mbeya DC), Kipembawe(Chunya DC), Mahongole(Mbarali DC), Lufilyo(Busokelo DC) na Ndanto(Rungwe DC) na ujenzi umekamilika.

### 7.8. Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

Mwaka 2019/2020 Mkoa wa Mbeya ulitenga Tshs. bil. 11,932,836,467.82 Kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya ikiwa ni pamoja na Ujenzi wa jengo la EMD.

Aidha, kuanzia Mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 Mkoa ulipokea Tshs. bil. 9,807,397,301.82 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya ikiwa ni pamoja na kuongeza majengo ya kutolea huduma za afya, ununuzi wa Mashine za kisasa za CT Scan, Digital X Ray, Mtambo wa Kuzalishia hewa tiba "Oxygen Plant", ununuzi wa Vifaa na Vifaa tiba vya Kisasa ambapo kwa sasa ujenzi umekamilika.

## SEKTA YA MAJI.

### 8.1 Huduma za Maji Vijijini

Mkoa una Mamlaka 5 za Maji safi na Usafi wa Mazingira mijini na Kamati za maji 328, Vyombo vya watumia maji ngazi ya jamii 111 (CBWSO).



Ujenzi wa Jengo la OPD na wodi grade A lililojengwa kwa Fedha za Serikali Kuu katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.




# ZIJUE FURSA 18 ZA UWEKEZAJI NDANI YA MKOA WA MBEYA



**MRADI WA UJENZI WA SHULE MPYA YA MSINGI TON YA KWA FEDHA ZA BOOST WENYE THAMANI YA TSH. 538,500,000**

Mahitaji ya maji kwa wakazi waishio vijijini ni wastani wa lita 58,845,920 kwa siku na mijini ni lita 92,144,760 kwa siku.

8.2 Hali ya Upatikanaji wa Maji Vijijini.

Hali ya upatikanaji wa maji vijijini imefikia asilimia 66.1 sawa na ongezeko la asilimia 6.4 kutoka kiwango cha asilimia 59.7 kilichokuwepo mwaka 2015.

8.3 Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini kwa mwaka wa fedha 2021/22

Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika Mkoa wa Mbeya kwa mwaka 2021/22 ni Tshs. bil. 13,350,289,025.00.

Aidha, hadi kufikia Juni, 2022 Jumla ya Tshs. bil. 12,609,828.500.00 zilipokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji mijini na vijijini.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23 RUWASA iliendelea kutekeleza jumla ya miradi ya maji 19 yenye thamani ya Tshs. bil. 38,773,137,747.27 hata hivyo hadi kufikia Juni 30, 2023 utekelezaji wa jumla ya miradi 12 yenye thamani ya Tshs. bil. 13,224,844,032.42 ilikamilika ambapo kati ya miradi hiyo, miradi 16 ni ya ujenzi, upanuzi na ukarabati huku miradi 3 ikiwa ni ya usanifu.

### 8.4 Bajeti na Mapokezi ya Fedha kwa ajili ya Miradi ya Maji Vijijini

Mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya Tshs. bil. 8,609,987,232.27 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza wa miradi mbalimbali ya maji vijijini ndani ya Mkoa wa Mbeya hata hivyo, hadi kufikia Juni 30, 2023 jumla ya Tshs. bil. 13,228,311,376.81 zilipokelewa ikiwa ni fedha za Mfuko wa Maji kwa ajili ya kutekeleza miradi inayotekelezwa kwa watalaamu wa ndani Force Account na Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji iliyo chini ya RUWASA ndani ya Mkoa.

### 8.5 Hali ya Upatikanaji wa Maji Jiji la Mbeya na Miji Mingine (MBEYAUWSA).

Mamlaka ya Maji Jiji la Mbeya ina jumla ya vyanzo 16 vyenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 59.5 kwa siku, uzalishaji halisi wa maji kwa siku ni wastani wa lita milioni 46.5 sawa na asilimia 78 ya mahitaji.

### 8.6.Utekelezaji wa Miradi ya Maji (MBEYA UWSA) kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetekeleza na kukamilisha miradi 6 yenye thamani ya Tshs. bil. 10.853. Miradi hii imeongeza uwezo wa kuzalisha maji kwa Lita milioni 28 kwa siku.

### 8.7.Utekelezaji wa Miradi ya Maji (MBEYA UWSA) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itakamilisha ujenzi wa miradi mitatu ya maji kwa gharama ya Tshs. bil. 6.2. Miradi hii itaongeza uwezo wa kuzalisha maji kwa lita milioni 4 kwa siku. Miradi hiyo ni Itagano, Halinji na Simba.

### 8.8.Mradi wa maji Mto Kiwira.

Mradi huu ulisainiwa Februari 12, 2023 na mkandarasi akaanza kazi Aprili 3, 2023. Mradi mpaka ukamilike utagharimu Tshs. bil. 119 na mkandarasi ni kampuni ya ujenzi ya China Railway Construction Engineering Group na kwamba ujenzi wa mradi ni wa miaka 2 kuanzia mwaka 2023 hadi 2025.

Mradi ukikamilika utakuwa unatoa kiasi cha lita milioni 117 kwa siku na kuongeza uzalishaji wa maji hadi kufikia lita milioni 184 kwa siku ukilinganisha na lita 66.5 zinazozalishwa sasa. Mradi utaweza kuwafikia wananchi zaidi ya asilimia 95 ifikapo mwaka 2025.

### 9. SEKTA YA NISHATI.

### 9.1. Hali ya Umeme katika Mkoa wa Mbeya.

Mkoa wa Mbeya unapata umeme wa Grid kupitia kwenye kituo cha Mwakibete ambacho kina mashine umba (transformer) mbili zenye uwezo wa jumla ya 150 MVA na mahitaji ya Mkoa ni MVA 87.52.

Mkoa una jumla ya laini za msongo wa kati (33kV & 11kV) zenye urefu wa kilomita 3,118.64 msongo mdogo (0.4kV & 0.23kV) zenye urefu wa kilomita 3,698.72, Transfoma 1,326 ambazo zinasambaza umeme.

### 9.3. Miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

Mradi huu wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili (REA III Round II) unatekelezwa kwenye vijiji 139 vya Mkoa wa Mbeya na mpaka sasa mkandarasi amewasha umeme kwenye vijiji 89 vya mradi. Na mpaka sasa wananchi 869 wameunganishwa na huduma ya umeme kwenye mradi huu.

Mradi huu una thamani ya Tshs. bil. 40.8 na gharama hizi ni kwa mkataba wa Mkoa wa Mbeya na wilaya zake zote. Mradi huu ni wa mkataba wa miezi 26 na utekelezaji wake unaendelea.

### 9.4. Mradi wa ujazilizi (Densification 2A)

Mradi huu wa ujazilizi (Densification 2A) unatekelezwa kwenye vitongoji 192 vya Mkoa wa Mbeya na mpaka sasa mkandarasi amewasha umeme kwenye vitongoji vyote 192 vya mradi. Na mpaka sasa wananchi 14,982 wameunganishwa na huduma ya umeme kwenye mradi huu na zoezi la kuwaunganishia umeme wananchi waliofikiwa na mradi linaendelea kufanyika kwa Mkoa mzima wa Mbeya. Mradi huu wa Densification 2A una thamani ya Tshs. bil. 23,491,978,702.88 kwa mkataba wa Mkoa mzima wa Mbeya.

### SEKTA YA BARABARA

### 10.1.WAKALA WA BARABARA NCHINI (TANROADS)

Ofisi ya Meneja wa Wakala ya Barabara (TANROADS) Mkoa wa Mbeya inahudumia barabara zenye jumla ya urefu wa km 1,403.34 zikijumuisha km 571.54 za barabara Kuu, km 686.16 za barabara za Mkoa, km 21.6 za barabara zilizopandishwa daraja na km 124.04 za barabara zilizokasimiwa. Mtandao huu wa barabara unajumuisha km 469.33 za barabara za lami sawa na asilimia 33.44% na km 934.01 za barabara za changarawe sawa na asilimia 66.56.

### Ujenzi wa njia ya kutua na kurukia ndege (runway) Songwe Airport



**Ujenzi wa wodi ya wanaume katika Hospitali ya wilaya ya Mbarali iliyojengwa kwa Fedha za Serikali Kuu**



**Ukamilishaji wa Majengo mapya na ununuzi wa samani katika Hospitali ya Jiji Igawilo wenye Thamani ya Tsh 1,300,000,000 kwa fedha za Serikali kuu**




**Mradi wa Maji Kijiji cha Sangambi Halmashauri ya Wilaya ya Chunya uliotekelezwa kwa fedha za UVIKO 19 katika mwaka 2021/22.**




# Zijue fursa 18 za uwekezaji ndani ya Mkoa wa Mbeya



Zao la Mpunga Mbarali DC




Zao la Mpunga Mbarali DC

Mkataba wa Ujenzi wa Kiwanja cha ndege Songwe ulisainiwa Agosti 30, 2019 kati ya TANROADS Makao Makuu kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mkandarasi China Geo- Engineering Corporation ya China. Gharama za mradi ni Tshs. bil. 14.758 bila VAT, mradi huu umekamilika.

**d. Ujenzi wa jengo jipya la abiria (terminal building) katika uwanja wa ndege wa Songwe.**

Ujenzi wa jengo la abiria unatekelezwa na Mkandarasi M/s China Geo-Engineering Corporation kwa gharama ya Tshs. bil. 14.118 bila kodi na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri M/s UNETEC kutoka Dubai. kwa sasa Mkandarasi anaendelea na kazi ya umaliziaji wa jengo hili.

Ujenzi wa kituo cha huduma ya pamoja mpakani (osbp) katika eneo la Kasumulu/Songwe katika mpaka wa Tanzania na Malawi.

Mradi wa ujenzi wa Kituo cha Huduma ya Pamoja mpakani katika eneo la Kasumulu/Songwe katika mpaka wa Tanzania na Malawi unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mkopo uliotolewa na Benki ya Dunia na unajengwa na mkandarasi China Geo Engineering Corporation.

Mradi huu wenye thamani ya Tshs. bil. 26.426 unajengwa kupitia Tanroads ambaye ndiye mwajiri na unasimamiwa na kampuni ya kihandisi ya ECG Engineering Consultant Group S.A ya Misri ikishirikiana na Wakala wa Majengo (TBA) na Gharama ya Mhandisi Mshauri ni Tshs bil. 1.005.

**Ujenzi wa barabara ya njia nne (dual carriageway) 32 km kuanzia Uyole (Nsalaga) hadi Ifisi**

Ujenzi wa barabara hii ulitangazwa Juni 6, 2022 na Zabuni zilifunguliwa Oktoba 20, 2022 na kwamba tayari Mkandarasi alishapatikana na serikali ilisaini mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Njia nne (Nsalaga – Ifisi km 32) na Kampuni ya CHICO kwa gharama ya Tshs. bil. 138.727 na Mkandarasi ameshaanza kazi za awali kama ujenzi wa kambi (camp site) na kusafisha eneo la barabara zinazoendelea. Tayari Mkandarasi ameshalipwa malipo ya awali ya Tshs. bil. 10.873.

Ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Ibanda – Kiwira port (km28.0) na Kajunjumele – Itungi port (km 4.0)

Mkandarasi tayari alishapatikana na mkataba ulisainiwa Desemba 27, 2022 na mradi huo utagharimu Tshs. bil. 38.359 na utatekelezwa na Kampuni ya AVM Delighan ya Uturuki na ameshalipwa malipo ya awali ya Tshs. bil. 3.8.

1.Mradi wa ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Igawa hadi Tunduma (km 218) na barabara ya mchepuko (Uyole bypass) kutoka Mlima nyoka hadi Songwe (km 48.0) katika barabara kuu ya TANZAM, kwa mfumo wa EPC+F

Mradi huu ulisainiwa Juni 16, 2023 na unatekelezwa kwa mfumo wa EPC+F yaani Usanifu, Manunuzi, Ujenzi na Gharama/Fedha (Engineering, Procurement, Construction and Finance) na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

Mradi unatekelezwa na Mkandarasi M/s China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa gharama ya Tshs. trilioni 1.133 bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kwamba jumla ya Km 218 zitajengwa kwa njia nne kuanzia Igawa hadi Tunduma.

Pia njia ya mchepuo wa Mbeya Mjini kilometa 48 itajengwa chini ya mradi huu hivyo kwa Mkoa wa Mbeya pekee, jumla ya kilometa 163 zitajengwa kupitia mradi huu na utekelezaji wake utachukua muda wa miaka mitano na nusu (miezi 66).

**WAKALA WA BARABARA MIJINI NA VIJIJINI (TARURA)**

Mtandao wa Barabara za TARURA Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Mbeya una mtandao wa barabara wenye jumla ya kilometa 4,512.27, kati ya hizo barabara za lami ni kilometa 111.43 sawa na asilimia 2.47, barabara za changarawe ni kilometa 1,384.96 sawa na asilimia 30.69 huku barabara za udongo zikiwa ni kilometa 3,015.88 sawa na asilimia 66.84.

Miradi ya Maendeleo kupitia Fedha za Wahisani (EU) kwa mwaka wa Fedha 2021/22 hadi June, 2023.

Mwaka wa fedha 2022/23 Mkoa uliendelea na utekelezaji wa miradi ambayo haikukamilika mwaka wa Fedha wa 2020/2021 ili kuikamilisha. Utekelezaji wa miradi hiyo umegharimu Tshs. bil. 16,399,222,095.00 na barabara zenye urefu wa km 39 zimejengwa.

Barabara hizo ni barabara ya Inyara – Simambwe yenye urefu wa km 16.7 iliyogharimu Tshs. bil. 7,052,878,707 na utekelezaji wake umefikia asilimia 85, barabara ya Lupeta – Wimba – Izumbwe yenye urefu wa km 10.1 iliyogharimu Tshs. bil. 4,645,401,000 ambayo utekelezaji wake umefikia asilimia 78 na barabara hizi zipo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, kuna Barabara ya Masebe DSP – MpugusoTTC – Bugoba kibaoni yenye urefu wa Km 5 iliyogharimu Tshs. bil. 2,123,900,000 na Barabara ya Masebe - Bugoba – Lutete yenye urefu wa km 7.2 iliyogharimu Tshs. bil. 2,577,042,388 na utekelezaji wake umekamilika.

Utekelezaji wa miradi ya mwaka wa fedha 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/23 kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara Mkoa wa Mbeya ni Tshs. bil. 20,495,308,018.57. Barabara zilizofanyiwa matengenezo kwa viwango mbalimbali ni km. 677.47, makalavati yaliyojengwa ni 199, box kalavati 9 na madaraja yaliyojengwa ni 15.

Mapokezi ya Fedha za matengenezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Mkoa wa Mbeya hadi kufikia mwezi Juni, 2023 ulipokea Tshs. bil. 19,867,377,009.37 sawa na asilimia 97 ya bajeti yote kwa ajili ya kutekeleza wa miradi ya Matengenezo, Majimbo, Tozo ya Mafuta na Maendeleo. Utekelezaji wa miradi hadi sasa umefikia asilimia 95.

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI (NIRC)**

Sekta ya Kilimo hasa eneo la utekelezaji wa miradi ya Umwagiliaji, Mkoa wa Mbeya umetengewa jumla ya Tshs. bil. 98,341,092,725.16 kwa ajili ya miradi 8 ya Umwagiliaji na kwamba mpaka sasa Mkoa umepokea Tshs. bil. 11,594,863,801.25.

**UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.



Shule Mpya ya Sekondari ya Dr. Tulia Ackson Mwansasu iliyojengwa kwa fedha za Miradi ya SEQUIP katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya

Halmashauri zimeendelea kuchangia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mwaka 2021/2022 hadi kufikia Juni, 2022 jumla ya Tsh. bil. 2,912,745,029.00 zilichangiwa na kukopeshwa kwa vikundi husika.

Aidha, mwaka 2022/2023 hadi kufikia Juni, 2023 Halmashauri zilichangia jumla ya Tshs. bil. 2,765,506,378 kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ambazo pia zilikopeshwa kwa vikundi husika.

**MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI (TASAF)**

Katika utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu, Mkoa Mbeya una jumla ya Walengwa 51,441 kutoka katika Vijiji/Mitaa 520. Adha, Uhawilishaji fedha kwa Walengwa umekuwa ukifanyika kila baada ya miezi miwili.

Katika kipindi cha Januari, 2014 hadi Juni, 2023, jumla ya awamu 33 (na 38 kwa Mbarali) za malipo (windows) zimefanyika. Jumla ya Tshs. bil. 53,513,170,227 zilitumika kwa ajili ya shughuli za Mpango ikihusisha malipo kwa walengwa Tshs. bil. 47,551,120,733 na fedha za ufuatiliaji Tshs. bil. 5,962,049,494.

**13.6 HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA HALMASHAURI**

Mwaka 2021/22 Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. bil. 41,403,664,000 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ya ndani na hadi kufikia Juni 30, 2022 jumla ya Tshs. bil. 45,062,879,382.05 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 105.57 ya lengo.

Kwa mwaka huu wa 2022/2023, Halmashauri zimeidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. bil. 47,537,528,438.63 ambapo hadi Juni 30, 2023 Halmashauri zilifanikiwa kukusanya Jumla ya Tshs. bil. 49,888,558,371.49 ambazo ni sawa na asilimia 105 ya lengo.



Shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazofanyika Mkoani Mbeya

UHURU
ya Kijani

MAONI YA MHARIRI

## Fursa zilizopo Mkoa wa Mbeya zikisimamiwa vizuri maendeleo makubwa zaidi yatapatikana

Mkoa wa Mbeya ni moja kati ya mikoa minne iliyopo katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania ambao una Wilaya tano na Halmashauri saba.

Mkoa huu ambao ulianzishwa mwaka 1961 ulikuwa ukijulikana kwa jina la 'Southern Highland Province'.

Mbeya imebarikiwa kwa kuwa na hali ya hewa nzuri pamoja na fursa mbalimbali za kiuchumi na ardhi yenye rutuba nyingi ambayo mazao mengi ya chakula na biashara yanastawi vizuri.

Katika Mkoa huu, kuna fursa 18 za uwekezaji ambazo iwapo zitasimamiwa kikamilifu, uchumi wa Mkoa wa Mbeya pamoja na maendeleo ya mkoa utakua kwa haraka.

Ndani ya fursa hizo 18, pia kuna fursa za utalii ambazo iwapo zitasimamiwa na kutangazwa katika maeneo mbalimbali duniani kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan alivyoweza kuvitangaza vivutio mbalimbali kupitia Filamu ya Tanzania The Royal Tour ambayo iliiwezesha dunia na kuona namna ambavyo Tanzania imebarikiwa kuwa na vivutio vingii vya utalii, naamini watalii wataongezeka zaidi ya ilivyo sasa.

Pia kuna rasilimali za misitu, kilimo cha mazao mbalimbali pamoja na madini mengi ya dhahabu yanayopatikana katika Wilaya ya Chunya na kwamba kupitia madini hayo vijana wengi wameweza kuendesha maisha.

Aidha, Mkoa kwa asilimia kubwa wananchi wake wanategemea kilimo cha mazao mbalimbali pamoja na ufugaji kidogo.

Sambamba na hayo, Mkoa umebahatika kuwa na vyuo vinavyozalisha wataalamu katika nyanja mbalimbali, baadhi ya vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (MUST), VETA Kanda ya Kusini- Magharibi na Chuo cha Kilimo Uyole (MATI Uyole).

Hizo ni baadhi tu, lakini fursa ni nyingi katika mkoa wa Mbeya ambazo kama zitatangazwa na kusimamiwa vizuri Mkoa utakua kiuchumi na hatimaye ajira nyingi zitazalishwa na serikali itaendelea kunufaika kwa ongezeko la vyanzo vya mapato na kodi itaongezeka na maendeleo yatapatikana.

Kwa mantiki hiyo jitihada za makusudi na uzalendo wa hali ya juu kutoka kwa viongozi wa Mkoa ikiwa ni pamoja na wakuu taasisi zilizopo mkoani humo ili kuhakikisha wanazitangaza fursa hizo na Mkoa kwa ujumla na hatimaye wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi waweze kujitokeza na kwenda kuwekeza mkoani humo ili serikali na wakazi wa Mbeya waweze kunufaika na rasilimali za kiuchumi zilizopo.

Nina imani kuwa iwapo jitihada zitachukuliwa, Mkoa utabadilika kwa maana ya kuwa mkoa wa kitalii, kibiashara na maendeleo makubwa yatapatikana kuliko yaliyoko sasa na vyanzo vya mapato ya serikali vitaongezeka ikiwa ni pamoja na ajira.

**Uhuru Publications Limited (UPL)**
S.L.P. 9221, Dar es Salaam
Makao Mkuu: Mtaa wa Lumumba Mkabala na Shule ya Msingi Mnazi Mmoja
Chumba cha Habari:
+255-739 957 882/FAX: 2183780
email: uhurunews@yahoo.com
uhuruadvert@gmail.com
uhurumakala@gmail.com

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu: ______ 0655 - 355810
Naibu Mhariri Mtendaji: ______ 0784 - 599717
Mhariri wa Habari: ______ 0713 - 117177
Mhariri wa Makala: ______ 0754 - 305135
Mhariri wa Michezo: ______ 0652- 161414

IDARA YA BIASHARA
Meneja Biashara UPL: ______ 0754 - 313140
Meneja Matangazo: ______ 0765 - 142207
Meneja Mauzo na Usambazaji: ______ 0683 - 378522

UHURU FM (PMCL)
uhurufmnews@gmail.com
Kaimu Mkurugenzi Uhuru FM: ______ 0765 – 383757
Kaimu Mhariri Mkuu Uhuru FM: ______ 0713 - 248640
Meneja Masoko Uhuru Fm: ______ 0715 – 584150

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Mkoa wa Mbeya

# WASIFU WA MKOA WA MBEYA

Mkoa wa Mbeya ni moja kati ya mikoa minne (4) iliyopo katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania. Mikoa mingine ni Rukwa, Iringa na Ruvuma. Mkoa wa Mbeya ulianzishwa mwaka 1961 na ulikuwa ukijulikana kwa jina la 'Southern Highland Province' kwa kujumuisha baadhi ya maeneo ya mikoa ya Iringa na Rukwa. Mkoa una eneo la kilometa za mraba 63,617, kati ya hizo kilometa mraba 61,783 ni za nchi kavu na kilometa za mraba 1,834 ni eneo la maji.

Kulingana na Sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 1967 mkoa ulikuwa na watu 969,053, Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 Mkoa wa Mbeya ulikuwa na jumla ya watu 2,063,328.

Kufikia mwaka 2010 mkoa ulikadiriwa kuwa na watu 2,662,156. Mkoa wa Mbeya upo Kusini Magharibi mwa eneo la Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania. Mkoa upo katika Latitudi kati ya 7º na 9º 31' Kusini ya Ikweta na Longitudo kati ya 32º na 35º Mashariki ya Greenwich.

Mkoa unapakana na nchi za Zambia na Malawi upande wa Kusini, Mkoa wa Rukwa upande wa Magharibi, Mikoa ya Tabora na Singida kwa upande wa Kaskazini ambapo kwa upande wa Mashariki unapakana na Mkoa wa Iringa.

> **"Mkoa unapakana na nchi za Zambia na Malawi upande wa kusini, Mkoa wa Rukwa upande wa magharibi, Mikoa ya Tabora na Singida kwa upande wa kaskazini ambapo kwa upande wa mashariki unapakana na Mkoa wa Iringa.**

Mji wa Tunduma katika Wilaya ya Mbozi na Kasumulu katika Wilaya ya Kyela, hufanya milango ya kuingilia na kutokea nchi za Zambia na Malawi.

Katika enzi za ukoloni wa Waingereza, Mkoa wa Mbeya ulikuwa ukijulikana kwa jina la 'Southern Highland Province'. Mkoa ulikuwa ukiunganisha baadhi ya maeneo ya mikoa mitatu ya sasa ambayo ni Iringa na Rukwa.

Jina la Mbeya limetokana na neno la kisafwa."Ibheya" ambalo maana yake ni chumvi, kutokana na wafanyabiashara kufika na kubadilishana mazao yao kwa chumvi.

Mji wa Mbeya ulianzishwa na wakoloni Waingereza mnamo mwaka 1927. Wakati huo dhahabu ilianza kupatikana katika milima iliyopo karibu na Mbeya hadi Chunya, hivyo Mbeya ulikuwa ni mji wa mapumziko kwa Wazungu kutokana na hali yake nzuri ya hewa, hali iliyosababisha mji wa Mbeya kupewa jina la utani kama "The Scotland of Africa" baada ya kutambua kama uoto, hali yake ya hewa na muonekano wa milima (hills) inayouzunguka mji wa Mbeya kufanana na Scotland mfano uoto unaopatikana katika mlima Loleza. Mkoa huu ni moja kati ya mikoa mikongwe

iliyokuwepo mpaka wa kati wa uhuru mwaka 1961. Katika kipindi hicho, makabila makuu katika Mkoa wa Mbeya yalikuwa ni Wasafwa, Wanyakyusa, Wandali, Wasangu, Wamalila, Wanyiha, Wakimbu na Wanyamwanga. Jamii hizo ni maarufu kwa kujishughulisha na kilimo na ufugaji mdogo mdogo.

## TANROADS - MKOA WA MBEYA

# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOTEKELEZWA NA TANROADS - MKOA WA MBEYA

**Na KOKU DAVID-**
*MBEYA.*

(i) **UJENZI WA BARABARA YA NJIA NNE (DUAL CARRIAGEWAY) 29KM KUANZIA UYOLE (NSALAGA) HADI IFISI**

Mkataba wa ujenzi wa Barabara hii yenye urefu wa kilometa 29 ya njia nne kuanzia Nsalaga – Ifisi ulisainiwa tarehe 14/02/2023. Mradi unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 unatekelezwa na Mkandarasi M/s China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) kwa gharama ya shilingi Bilioni 138.727 bila kodi ya ongezeko la thamani (VAT) Mkandarasi amemaliza ujenzi wa kambi yake kwa asilimia 100% na upande wa kambi ya Mhandisi Mshauri ujenzi umefikia asilimia 70%. Kazi za Ujenzi wa barabara imefikia asilimia 4. Mradi huu ni wa miaka miwili na inategemewa kuwa utakamilika tarehe 13 Machi, 2025. Mara baada ya kukamilika mradi huu utapunguza sana msongamano wa magari katika Jiji la Mbeya na pia utakuza uchumi wa Mkoa na Jamii kwa ujumla.

**Utekelezaji wa Barabara ya Ujenzi wa Njia Nne Mkoani Mbeya**

(ii) **UKARABATI KWA KIWANGO CHA LAMI BARABARA YA IBANDA – KIWIRA PORT (KM28.0) NA KAJUNJUMELE – ITUNGI PORT (KM 4.0)**

Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 27 Desemba 2022. Gharama ya mradi ni Shilingi 38.359 bilioni bila nyongeza za thamani (VAT) na utatekelezwa na Kampuni ya AVM-Dilligham ya Uturuki. Muda wa utekelezaji ni miezi 24. Hadi kufikia sasa mkandarasi ameanza kusafisha maeneo ya kufanya kazi na anaendelea na Ujenzi wa kambi (camp site)

**2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KATIKA ENEO LA INYALA**

**2.1: Kuimarisha Barabara ya Mchepuko (Detour Road)**

Kazi ilianza tarehe 22 Desemba, 2022 na kumalizika tarehe 22 Juni 2023. Mkandarasi aliyetekeleza kazi hii ni (China Geo-Engineering Corporation) kwa gharama ya shilingi Billioni 7.0 kazi zimekamilika kwa asilimia 100 kulingana na mkataba/aina ya matengenezo yanayotakiwa. Lengo la kazi hii ni kuchepusha magari katika mlima Inyala ili kuepusha ajali.

Picha ikionyesha muonekano wa Barabara ya Mchepuko (Detour Road) eneo la Inyala baada ya kukamilika kwa Ujenzi huo.s

(iii) **UJENZI WA JENGO JIPYA LA ABIRIA (TERMINAL BUILDING) KATIKA UWANJA WA NDEGE WA SONGWE.**

Ujenzi wa jengo la abiria (Terminal Building) unatekelezwa na Mkandarasi M/s China Geo-Engineering Corporation kwa gharama ya bilioni 14.118 bila kodi na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri M/s UNETEC kutoka Dubai. kwa sasa Mkandarasi anaendelea na kazi ya ukamilishaji wa jengo na limekamilika kwa asilimia 98.85

Utekelezaji wa jengo jipya la abiria (Terminal Building) katika uwanja wa ndege wa songwe.

(iv) **UJENZI WA TAA ZA KUONGOZA NDEGE KATIKA NJIA YA KUTUA NA KURUKA NDEGE SONGWE AIRPORT.**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliingia mkataba wa kuweka taa tarehe 6 Julai, 2017 kwa gharama ya Shilingi Bilioni 4.688 na Mkandarasi GECI Espanola S.A wa Spain. Hadi kufikia mwezi Septemba, 2022 Mkandarasi alikuwa amekamilisha kazi zote za kusimika miundombinu ya taa (civil works) katika njia ya kutua na kuruka Ndege (Runway) na mpaka sasa kwa ujumla mradi umekamilika kwa asilimia 100% na taa zinawaka

Utekelezaji wa usimikaji wa taa za kuongoza ndege wakati wa kutua na kuruka uwanja wa ndege Songwe.

(v) **UJENZI WA NJIA YA KUTUA NA KURUKIA NDEGE (RUNWAY) SONGWE AIRPORT**

Mkataba wa Ujenzi wa Kiwanja cha ndege Songwe ulisainiwa tarehe 30 Agosti, 2019 kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Makao Makuu kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mkandarasi China Geo- Engineering Corporation ya China. Gharama za mradi ni shilingi Bilioni 14.758 bila VAT, Muda wa kazi ni miezi nane pamoja na mwezi mmoja wa maandalizi na Msimamizi wa mradi huu ni TANROADS - Mbeya. hadi Septemba, 2022 Mkandarasi alikuwa amemaliza ujenzi huu kwa asilimia 100% na njia ya kuruka ndege (runway) imeanza kutumika.

Utekelezaji wa ujenzi wa njia ya kutua na kurukia ndege (Runway) uwanja wa ndege wa Songwe



Ujenzi wa barabara ya Mchepuo iliyojengwa eneo la Inyala Wilaya ya Mbeya



Mradi wa Taa za kuongozea ndege katika Uwanja wa Ndege wa Songwe






Ujenzi wa barabara njia nne Mbeya Mjini



(vi) **UJENZI WA KITUO CHA HUDUMA YA PAMOJA MPAKANI (OSBP) KATIKA ENEO LA KASUMULU/ SONGWE KATIKA MPAKA WA TANZANIA NA MALAWI.**

Mradi wa ujenzi wa kituo cha huduma ya Pamoja mpakani katika eneo la kasumulu/Songwe katika mpaka wa Tanzania na Malawi unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mkopo uliotolewa na Benki ya Dunia na unajengwa na mkandarasi China Geo Engineering Corporation.

Mkataba wa Mradi huu ulisainiwa tarehe 12 Juni 2019 na mkandarasi alianza kufanya kazi tarehe 01 Oktoba 2019.

Mradi huu wenye thamani ya shilingi za kitanzania bilioni 26.426 unajengwa kupitia Wakala wa Barabara (Tanroads) ambaye ndiye mwajiri na unasimamiwa na kampuni ya kihandisi ya ECG Engineering Consultant Group S.A ya Misri ikishirikiana na Wakala wa Majengo (TBA) na Gharama ya Mhandisi Mshauri ni shilingi za kitanzania bilioni 1.005.

Hadi kufikia Septemba, 2023, Mkandarasi alikua ameshafanya kazi kwa asilimia 90.4% na kulipwa jumla ya shilingi bilioni 21.922 kupitia hati za malipo zilizoidhinishwa ambayo ni sawa na asilimia 90%

Pamoja na hayo, malipo ya fidia ya kupisha ujenzi yenye jumla ya shilingi bilioni 5.779 yalishalipwa kwa wananchi wote wanaostahili

**UJENZI WA KITUO CHA HUDUMA YA PAMOJA MPAKANI (OSBP) KATIKA ENEO LA KASUMULU/SONGWE KATIKA MPAKA WA TANZANIA NA MALAWI.**

(vii) **UJENZI WA BARABARA YA KATUMBA – MBAMBO – TUKUYU (KM 81) KWA KIWANGO CHA LAMI, SEHEMU YA BUJESI - MBAMBO (KM10) NA TUKUYU - MBAMBO (KM 7)**

Baada ya kukamilika kwa Ujenzi wa eneo la Lupaso – Bujesi km (10.0) ambao ulipokelewa tarehe 02 January 2019 baada ya kipindi cha matazamio kukamilika. Mradi wa kiwango cha lami eneo lililobaki (km 71) unaendelea kutekelezwa kwa kipande cha Bujesi - Mbambo (km 10) na Tukuyu - Mbambo (km 7.)

Hivi sasa mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii na kwa sasa kiasi cha utekelezaji ni asilimia 97.0%. Msimamizi wa mradi huu ni Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mbeya na mradi unatekelezwa na mkandarasi China Railway 15 Bureau Corporation No 666 kutoka China kwa jumla ya gharama ya shilingi bilioni 21.307 bila kodi.

Sehemu ya Katumba - Lupaso (km 35.3) na Mbaka - Kibanja (km 20.7) tayari mchakato wa Manunuzi unaendelea.

Picha ikionyesha utekelezaji wa Barabara ya Katumba – Mbambo - Tukuyu

**2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI KATIKA ENEO LA INYALA**

2.1: Kuimarisha Barabara ya Mchepuko (Detour Road)

Kazi ilianza tarehe 22 Desemba, 2022 na kumalizika tarehe 22 Juni 2023. Mkandarasi aliyetekeleza kazi hii ni (China Geo-Engineering Corporation) kwa gharama ya shilingi Billioni 7.0 kazi zimekamilika kwa asilimia 100 kulingana na mkataba/aina ya matengenezo yanayotakiwa. Lengo la kazi hii ni kuchepusha magari katika mlima Inyala ili kuepusha ajali.

Picha ikionyesha muonekano wa Barabara ya Mchepuko (Detour Road) eneo la Inyala baada ya kukamilika kwa Ujenzi huo.c







# KAPUNGA RICE PROJECT LIMITED:
## TUMECHANGIA KUIFANYA TANZANIA KUWA MIONGONI MWA NCHI ZINAZOONGOZA KUZALISHA MCHELE BARANI AFRIKA

**Na KOKU DAVID-** *Mbarali*




**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan alipoweka jiwe la msingi wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Afya cha Kapunga Julai 29, 2018, kilichojegwa na Mwekezaji Kapunga Rice Project Limited.**

Mwaka 1992 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishauriwa na Benki ya Dunia kutekeleza sera za Ubinafsishaji na kwamba sera hizo zinawahitaji wawekezaji na wenye mitaji mikubwa kuwekeza nchini kwenye viwanda na mashamba makubwa ili kuweza kuzalisha mahitaji na kujitosheleza kwa chakula.

Mwanzoni, Watanzania waliona Ubinafsishaji ni kama dawa chungu na itakayowanyang'anya wananchi miliki ya njia kuu za uchumi. Lakini hivi sasa ni takribani miaka 30 ya utekelezaji wa sera hizo na kumekuwa na mafanikio makubwa yaliyopatikana na ambayo yameifanya nchi kujitosheleza kwa chakula pamoja na nchi majirani.

Mratibu wa kampuni ya Kapunga Rice Project Limited (KRPL) iliyopo wilayani Mbarali mkoa wa Mbeya Sunil Tayil, analiambia gazeti la Uhuru ya Kijani kuwa nafaka wazalisha kwa kiwango kikubwa hadi kuwa na ziada ni mchele.

Anasema ripoti ya shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) inaonesha kuwa mahitaji ya mchele duniani ni tani milioni 500 wakati uzalishaji wake ni tani milioni 480 na kwamba takwimu hizo zinabainisha wazi kuwa soko la mchele duniani lilivyo kubwa.

Anasema kampuni yao ni miongoni mwa wawekezaji wenye mchango mkubwa kwa Taifa na kwamba kwa Zaidi ya miaka kumi ya uwekezaji walioufanya, wamechangia kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kuzalisha mchele kwa kiasi kikubwa barani Afika.

Uendelezaji wa shamba la mpunga la Kapunga unafanyika kitaalamu na kwamba shamba hilo wakati linabinafsishwa kwa kampuni hiyo lilikuwa na ukubwa wa hekta 7370 lakini baadae mwaka 2016 serikali ilikubaliana na mwekezaji kutoa hekta 1870 na kuwapa wananchi wa kijiji cha Kapunga na kulifanya shamba hilo kubaki na ukubwa wa hekta 5500.

**UENDELEZAJI WA SHAMBA LA MPUNGA LA KAPUNGA.**

Tayil anasema kampuni yake ilianza kulima mpunga mwaka 2007 kwenye eneo la hekta 350 zilizofaa kulimwa kwa wakati huo na kufanikiwa kupata mavuno ya chini ya tani moja kwa hekta na kwamba hekta nyingine 2250 zilishindikana kulimwa kutokana na kuwa zilihitaji ukarabati mkubwa.

Anasema kufikia msimu wa mwaka 2011/12 kampuni hiyo ilifanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya shamba pamoja na kinu cha kukobolea mpunga ambacho ni miongoni mwa vinu vikubwa barani Afrika.

Anasema, pia walifanya ukarabati wa miundombinu ya mifereji ya umwagiliaji na usawazishwaji wa ardhi mashambani kwa zaidi hekta 3500.

Mafanikio yaliyopatikana baada ya uwekezaji huo mkubwa.

Tayil anasema kutokana na uwekezaji huo mkubwa walioufanya, kupitia serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mh. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania shamba la Kapunga lilifanya utafiti na kufanikiwa kuunganisha kilimo cha kisasa na kile cha asili hali iliyosaidia wakulima wadogo na wa kati kuwa na mahusiano mazuri na wakulima wakubwa.

Anasema mafanikio mengine ni kwamba kazi zote za ulimaji mpunga kwenye eneo hilo kufanywa na mashine za kisasa zenye teknolojia mpya kuanzia kulima na kusawazisha ardhi, upandikizaji, upuliziaji dawa kuua magugu na wadudu, uwekaji mbolea na hadi kufikia hatua ya kuvuna mpunga lakini pia kuhifadhi katika maghala na usindikaji kimataifa.

"Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana toka mwaka 2007 baada ya shamba hilo kukabidhiwa kwa kampuni ya Kapunga ni kuweza kuinua kiwango cha uzalishaji kutoka kilo 800 kwa kila hekta moja na kufikia kilo 7,200 kwa hekta moja.

"Mafanikio haya yamechangiwa na mazingira mazuri tuliyotengenezewa na serikali ya ubia kati yake na wawekezaji," anasema Tayil.

Anasema Kapunga imekuwa mstari wa mbele kuwawezesha wakulima wadogo kushiriki katika kilimo cha mpunga kwa kulima kwa kushirikiana kwa pamoja.

Anasema Jumla ya hekta 1,165 zimelimwa na wakulima waliovutiwa na mpango huo huku wakulima 350 wakiwa wamejisajili na wengi kunufaika kwa namna moja na kwamba wafanyabiashara na wawekezaji wadogo ni wanufaika wa kilimo hicho.

Anasema katika kuwasaidia, kampuni huwalimia wakulima mashamba yao na kuwapatia mbegu bora zilizofanyiwa utafiti hapa nchini pia huwapatia mbolea na madawa, kuwapa msaada wa ushauri wa kitaalamu, kuwapatia huduma za umwagiliaji na uvunaji kwa mashine.

Anaongeza kuwa mchango wa mkulima ni kupandikiza shamba lake na kulitunza hadi wakati wa mavuno na baada ya mavuno Kampuni huchukua mpunga kwa mkulima kulingana na makubaliano kati ya Kampuni na wakulima yaliyofanyika kabla ya msimu wa kilimo kuanza.

Aidha, kiasi kinachobakia huchukuliwa na mkulima kwa ajili ya kwenda kuhifadhi au kuuza na kwamba wastani wa kipato katika kila shamba moja la ekari 15 ni tani 42.

Kutokana na faida inayopatikana, anasema kuwa makundi mengi ya wakulima wamejitokeza kwa wingi ili kuomba kuingia katika mpango huo.

Anasema kazi inayofanywa na serikali ya Rais wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan ya kufikisha pembejeo kwa wananchi kabla ya msimu na mazingira ya upatikanaji wake kwa bei ya ruzuku imechochea uzalishaji wa mpunga kwa wingi hali iliyochangia nchi za Kenya, Uganda Zambia na Jamuhuri ya Kidemokrasi ya Kongo kuwa wanunuzi wao.

Aidha, mbali na ongezeko la uzalishaji wa zao la mpunga shamba hilo limeweza kuchangia katika kutoa ajira za kudumu kwa Watanzania zaidi ya 115 ambao wameajiriwa huku Idadi ya wataalamu wa kigeni 10 kutoka India na Bangladesh nchi zinazoongoza kuzalisha mpunga duniani nao wameajiriwa.

Tayil anasema shamba hilo huajiri vibarua wa muda zaidi ya 3000 kila msimu unaoanzia mwezi Novemba hadi July kila mwaka na kwamba ukichanganya na idadi ya vibarua wanaofanya kazi kwenye mashamba ya wakulima katika mpango wa uchangiaji inafikia vibarua 5000 kila msimu.

Anasema vibarua wanaofanya kazi katika mashamba ya Kapunga ambao hutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania, huenda kufanya kazi hizo ili waweze kuendesha maisha yao ikiwa ni pamoja na kuweza kutimiza malengo yao na kwamba fedha wanazozipata kutokana na kazi hizo zimewawezesha kujenga nyumba bora na kuhudumia familia zao.

"Shamba la Kapunga limekuwa chachu ya ustawi kwa vijiji vilivyo Jirani na shamba hilo na kwamba zaidi ya wakazi 10,000 na familia zao wamenufaika na kuweza kuinua hali za maisha yao.

"Lakini pia, ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao yanayomilikiwa na wakulima umeshamiri sambamba na nyumba bora za kuishi na biashara, pia vinu vya kukobolea mpunga vinavyomilikiwa na wakulima vimetapakaa huku shughuli nyinginezo za biashara zikiendelea kwenye vijiji hivyo usiku na mchana na kwamba iwapo hali itaendelea hivi bila shaka kijiji cha Kapunga kitakuwa mji mdogo kama ilivyo Chimala," anasema Tayil.

Anasema ustawi wa vijiji hivyo umeusukuma uongozi wa kampuni ya Kapunga kujitosa kusaidia shughuli nyingine za kijamii ili kuwapunguzia kero ambapo imejenga shule ya msingi ya kisasa katika kitongoji cha Site One kwa gharama ya Zaidi ya milioni 550 hali ambayo imeondoa tatizo la watoto kutembea umbali mrefu kufuata shule.

Sambamba na hilo, pia imekamilisha ujenzi wa zahanati ya kisasa iliyojengwa kwenye kitongoji cha Mapogoro iliyogharimu zaidi ya Tshs. milioni 750 na kuzinduliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Pia kampuni hiyo imekarabati mfumo wa maji ya bomba uliogharimu zaidi ya Tshs. milioni 20 na kuondoa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa Kapunga.

Kampuni hiyo pia imekarabati kituo cha Polisi cha Chimala kilichopo kilometa 26 toka shamba la Kapunga lilipo ikiwa ni pamoja na kuchangia ujenzi wa ofisi ya serikali ya kijiji cha Kapunga.

Changamoto.

Pamoja na mafanikio mbalimbali iliyopata Kampuni ya Kapunga, imekuwa ikikabiliwa na changamoto za uwepo wa kodi kubwa za ushuru wa pembejeo na mashine za kilimo hali inayosababisha wananchi kushindwa kuingia kwenye kilimo cha kisasa hivyo ni vema serikali ikaangalia upya namna ya kuwapunguzia.

Changamoto nyingine inayolikabili shamba hilo na vijiji vya Jirani ni uvuvi haramu, ufugaji holela, wezi wa maji na uharibifu wa mitaro ya umwagiliaji, mawasiliano duni ya simu na Ubovu wa barabara kutoka Chimala hadi Kapunga.

Tayil anasema kuwa kutokana na msimamo wa serikali kuhamasisha kilimo kumekuwa na ongezeko kubwa la watu kuingia wenye kilimo hali inayosababisha shamba la Kapunga kuanza kuelemewa na maombi kutoka kwa wakulima wanaotaka kufanya kilimo katika shamba hilo, hivyo viongozi na wataalamu wa ugani wanatakiwa kuwa karibu na wawekezaji wa kilimo ili kutafakari namna bora ya kuleta ufanisi.



**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alipotembelea na kukagua kiwanda hicho.**



**Kiwanda cha Kapunga Rice Project Limited.**



**Mashine ya uvunaji wa Mpunga**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
Improved Roads For Sustainable Development

## WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI-TANZANIA (TARURA)

## TAARIFA YA MAFANIKIO KATIKA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KIPINDI CHA AWAMU YA SITA YA SERIKALI JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA HADI OKTOBA, 2023 MKOANI MBEYA

### UTANGULIZI

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) Mkoa wa Mbeya inahudumia Halmashauri Saba (07). Halmashauri hizo ni Mbeya, Busokelo, Chunya, Kyela, Mbarali, Jiji la Mbeya na Rungwe. Lengo kubwa la kuanzishwa kwa TARURA ni kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati jukumu la menejimenti ya mtandao wa barabara za Wilaya lilipokuwa chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na pia kuendana na mabadiliko katika Sekta ya Barabara kwa nia ya kuboresha huduma na kuongeza ufanisi.

### MTANDAO WA BARABARA

Kuanzia mwaka 2021/2022 hadi Oktoba, 2023 Wakala Barabara Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), Mkoa wa Mbeya unahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya 4,512.24 km, Madaraja 371, Kalvati 3,015, Boksi Kalvati 488 na Madrifti 25. Kama inavyo oneka katika jedwali hapa chini.

### UREFU WA BARABARA NA IDADI YA MADARAJA, MABOKSI KALAVATI, MAKALAVATI NA MADRIFTI

| NA. | JINA LA HALMASHAURI | MTANDAO WA BARABARA (KM) | MADARAJA | MABOKSI KALAVATI | MAKALAVATI | MADRIFTI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Busokelo DC | 505.39 | 68 | 72 | 527 | 0 |
| 2. | Chunya DC | 580.49 | 19 | 5 | 518 | 8 |
| 3. | Kyela DC | 514.60 | 23 | 320 | 478 | 1 |
| 4. | Mbarali DC | 685.86 | 43 | 5 | 505 | 2 |
| 5. | Mbeya CC | 426.69 | 52 | 9 | 309 | 2 |
| 6. | Mbeya DC | 1,033.30 | 86 | 4 | 316 | 12 |
| 7. | Rungwe DC | 765.91 | 80 | 73 | 362 | 0 |
| JUMLA | | 4,512.24 | 371 | 488 | 3015 | 25 |

### MWENENDO WA BAJETI KWA MIAKA MITATU

Mwaka wa fedha wa **2021/2022** katika mwendelezo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020, kwenye Ibara ya 57(a) serikali ya CCM inayoongozwa na **Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamuru kuongeza bajeti ya Matengenezo ya barabara katika Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) katika mwaka wa Fedha **2021/2022.**

Kufuatia nyongeza hiyo ya fedha ya **Tshs Bilioni 9.759** Mkoa wa Mbeya uliidhinishiwa na kuletewa bajeti ya **Shilingi bilioni 17.959,** badala ya **shilingi Bilioni 8.2** ya mwaka wa fedha wa **2020/2021.**

Ongezeko hili ni sawa na a**silimia 119% ya bajeti ya 2020/2021.** Kiasi hicho cha fedha **(Tshs. Bilioni 17.958)** kilitumika kutengeneza barabara zenye urefu wa km **722.42** zilifanyiwa matengenezo, Madaraja **35** na makalavati **72** yalijengwa kwa mwaka wa fedha **2021/2022**.

Mwaka wa **Fedha 2022/2023, Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), akaamuru kuongeza tena kutoka **Bilioni 8.2** ya mwaka 2020/2021 na kuwa Shilingi **bilioni 23.542** Nyongeza hiyo ya fedha, **(Tshs Bilioni 15.342)** ni sawa na **asilimia 187%** ya bajeti ya 2020/2021.

Kiasi hicho cha fedha **(Tshs. Bilioni 23.542)** kilitumika kutengeneza barabara zenye urefu wa **km 718.88** zilifanyiwa matengenezo, Madaraja **24** na makalavati **199** yamejengwa kwa mwaka wa fedha **2022/2023.**

Mwaka wa Fedha **2023/2024**, **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), akaamuru kuongeza tena kutoka **Bilioni 8.2** ya mwaka 2020/2021 na kuwa Shilingi **bilioni 24.442** Nyongeza hiyo ya fedha, **(Tshs Bilioni 16.242)** ni sawa na **asilimia 198%** ya bajeti ya **2020/2021.**

### MIRADI MIKUBWA ILIYOTEKELEZWA KWA MIAKA MITATU YA AWAMU YA SITA – TARURA MKOA WA MBEYA

| Na. | Jina la mradi | Mahali ulipo | Gharama (TZS) | Manufaa ya mradi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa daraja la Tembela – Mwasanga lenye urefu wa 20m ikiwa ni Pamoja na ujenzi wa barabara za maingilio mita 500 kwa kiwango cha Lami. | Mbeya CC | 1,985,044,200.00 | Daraja linaunganisha Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Mbeya Vijijni. |
| 2 | Ujenzi wa Daraja la Mafumbo kwa kutumia Teknolojia ya kujenga madaraja kwa Mawe ikiwa ni pamoja na barabara zake za maingilio katika barabara ya Iwiji – Izyira Km 16 | Mbeya DC | 500,000,000.00 | Daraja linaunganisha Kijiji cha Iwiji na Kijiji cha Izyira na Mji wa Vwawa (Mbozi). |
| 3 | Ujenzi wa Daraja la Ngubuswi katika barabara ya Kisegese – Kasyabone – Ntaba. | Busokelo | 698,982,520.00 | Daraja linaunganisha Halmashauri ya Busokelo na Kyela. |
| 4 | Daraja la Ibungu la watembea kwa miguu (kiteputepu) lenye urefu wa mita 85. | Kyela DC | 79,000,000.00 | Daraja hili linaunganisha Kata za Ndandalo, Ikimba, Mikoroshini na Mji wa Kyela. |
| 5 | Ujenzi wa Barabara katika Mji wa Kyela 2.47km kwa kiwango cha Lami. | Kyela DC | 1,035,440,648.00 | Barabara bora zinarahisisha shughuli za jamii za kiuchumi, kijamii na Utawala na kupendezesha Mji wa Kyela na Jiji la Mbeya |
| 6 | Ujenzi wa barabara za Hospital Hill na Airport – Darajani 0.6km kwa kiwango cha Lami. | Mbeya CC | 693,640,600.00 | |
| 7 | Ujenzi wa barabara ya Wageni na barabara ya Independence kwa jumla ya 0.8km kwa kiwango cha Lami. | Mbeya CC | 808,280,515.00 | |
| 8 | Ukarabati wa Barabara ya udongo ya Ifumbo (km 10) "Earth Road" na kuwa Barabara ya Changarawe "Gravel Road". | Chunya DC | 485,185,000.00 | Barabara bora inarahisisha Shughuli za jamii za kiuchumi, kijamii na Utawala katika Halmashauri ya Chunya |

### BAADHI YA PICHA ZA BAADHI YA MIRADI ILIYOTEKELEZWA KWA KIPINDI HIKI CHA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023 HADI OKTOBA, 2023.





*Mbeya CC - Ujenzi wa Barabara za Lami katika Jiji la Mbeya.*



*Busokelo - Ujenzi wa Daraja la Lufilyo C katika Barabara ya Luteba - Kandete.*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI

# Zaidi ya bil. 160 zatekeleza miradi Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali



KANALI DENIS MWILA-MKUU WA WILAYA YA MBARALI



GODFREY KAWACHA-KATIBU TAWALA MBARALI

**Na KOKU DAVID-**
*Mbarali*

**UTANGULIZI**

WILAYA ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya tano na Halmashauri saba zinazounda Mkoa wa Mbeya. Wilaya hii ilianzishwa mnamo tarehe 7 Julai, 2000 kwa mujibu wa vifungu vya 8 na 9 vya Sheria ya Serikali za mitaa ya mwaka 1982 na kupatiwa cheti kilichosainiwa tarehe 5 June, 2003.

Wilaya ya Mbarali ipo kati ya nyuzi 33.40 na 35.40 Longitudo kuelekea upande wa Mashariki, nyuzi 7.41 na 9.25 kusini ya Ikweta. Upande wa Kaskazini Mashariki, inapakana na Wilaya ya Iringa Vijijini, upande wa Mashariki inapakana na Wilaya ya Njombe, upande wa Kusini kabisa inapakana na wilaya ya Mbeya na Kaskazini inapakana na Wilaya ya Chunya.

**WILAYA INA JUMLA YA ENEO LA KILOMETA ZA MRABA 16,000**

Wilaya ya Mbarali ipo katika latitude inayoanzia mita 1,000 – 1,800 juu ya usawa wa Bahari. Wastani wa joto ni kati ya nyuzi 25c na 30c. Wastani wa mvua hutofautiana kati ya milimita 300-940, hata hivyo kuna misimu miwili yaani msimu wa kiangazi ambao huanzia mwezi Mei – Novemba na msimu wa mvua ambao huanza Desemba – Aprili

Makabila makuu yaliyopo Wilayani Mbarali ni Wasangu, Wahehe, Wakinga, Wabena na Wanyakyusa. Vile vile yapo makundi madogo ya makabila wakiwemo Wasukuma, Wanji, Wabarbeig na Wagogo.

Makundi mengi ya makabila haya ni wakulima na wafugaji ambao walihamia bonde la Usangu kutoka Mikoa ya Arusha, Mwanza, Shinyanga, Singida na Dodoma.

Kufuatia sensa ya kitaifa ya idadi ya watu ya mwaka 2022, Wilaya ya Mbarali sasa ina jumla ya watu 446,336 ambao kati yao 217,280 ni wanaume na 229,056 ni wanawake ikiwa na ukuaji wa 4.0%.

**2. UTEKELEZAJI WA MIRADI.**

Hadi kufikia mwezi Septemba 30, 2023, Wilaya ya Mbarali imetekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kupitia sekta zilizopo chini yake ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 – 2025.

Mafanikio makubwa yameshuhudiwa katika Sekta za Elimu ya awali na Msingi, Elimu Sekondari, Afya, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, na maji ambapo jumla ya miradi yenye thamani ya Tshs. bil. 160,360,568,357.99 imeendelea kutekelezwa katika Sekta mbalimba za Wilaya ya Mbarali.

**ELIMU YA AWALI NA MSINGI.**

Elimu ya awali na msingi halmashauri ilipokea jumla ya Tsh 3,471,628,759.00 na kuwezesha ujenzi wa shule 2 mpya za awali kwa gharama ya Tshs. milioni 124,924,000, shule mpya za msingi 2 kwa gharama ya Tshs. milioni 511,500,000.00, madarasa mapya 108 kwa gharama ya Tshs. bil. 2,071,250,000.00, matundu ya vyoo 283 kwa gharama ya Tshs. milioni 389,000,000.00, nyumba 5 za walimu kwa gharama ya Tshs. milioni 200,000,000, huduma ya maji safi na salama (unawaji mikono) Tsh. milioni



TWALIBU LUBANDAMO-MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI



MISSANA KWANGURA-MKURUGENZI HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI




Jengo la Huduma za Dharura (EMD) lililojengwa kwa fedha za UVIKO 19 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.



# Zaidi ya bil. 160 zatekeleza miradi Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali

23,744,759.00, ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye uhitaji maalum Tshs. milioni 128,000,000.00 na ukarabati wa majengo mbalimbali katika halmashauri uliogharimu Tshs. milioni 23,210,000. Aidha jumla ya madawati 1725 na seti za meza na viti vya walimu 115 vimetengenezwa.

**ELIMU SEKONDARI.**

Jumla ya kiasi cha Tshs. bil. 4,313,180,028.00 kilipokelewa na halmashauri na kuwezesha ujenzi wa madarasa 143 kwa gharama ya Tshs. bil. 2,860,000,000.00, vyumba 8 vya maabara kwa gharama ya Tshs. bil. 240,000,000, Shule 2 mpya za sekondari kata ya Chimala na Rujewa kwa gharama ya Tshs. bil 1,053,180,028.00, nyumba ya mwalimu ya familia 2 katika shule ya sekondari Chifu Merere kwa gharama ya Tshs. milioni 100,000,000 na mabweni 2 katika shule ya sekondari Mapogoro na Igava kwa gharama ya Tshs. milioni 60,000,000.00.

**AFYA.**

Katika kipindi cha awamu ya sita uboreshaji wa huduma katika Sekta ya Afya umeimarika kwa kiwango kikubwa ambapo Jumla ya kiasi cha Tshs. bil. 4,015,000,000.00 kimepokeleawa na kuwezesha ujenzi wa majengo Matano ya hospitali ambayo ni jengo la huduma za dharula, wodi mbili za upasuaji, jengo la upasuaji, jengo la kuhifadhi maiti, vituo vya afya 3 (Mahongole, chimala na Igava), zahanati 10, ujenzi wa nyumba ya mtumishi ya familia tatu, ukarabati wa jengo la UVIKO na ununuzi wa vifaa tiba.

Aidha utoaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya zinaptika na kuna vituo 72 vya Afya.

**KILIMO, MIFUGO NA UVUVI.**

Halmashauri ya Mbarali imekuwa na mafanikio makubwa katika Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi yanayotokana na uwekezaji unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha miundombinu ya kilimo na mifugo ambapo jumla ya miradi yenye thamani ya Tshs. bil. 77,465,062,057.00 imetekelezwa katika Wilaya Mbarali.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa majosho kumi (10) yenye thamani ya TShs. milioni 230,000,000, Ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji kwenye shamba la malisho la Langwira kwa gharama ya TShs. milioni 203, 412,530, ujenzi wa mnada katika kata ya Utengule Usangu kwa gharama ya Tshs. milioni 468,516,262 na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu kumi (10) za umwagiliaji kwa gharama ya Tshs. bil. 76,563,133,265.

Skimu zinazojengwa ni Uturo na Isenyela kwa Tshs. bil. 13,927,976,600.00, Matebete na Gonakuvagogolo kwa Tshs. bil. 10,457,872,932.00, Chosi na Herman kwa Tshs. bil. 15,068,437,632.00, Msesule kwa Tshs. bil. 13,412,165,914.00, Madibira kwa Tshs. bil. 8,759,866,327.76, Mbuyuni na Makangalawe kwa Tshs. bil. 14,936,813,856.40. pia Serikali imeboresha huduma za ugani kwa kuwanunulia pikipiki 76 maafisa ugani.

**MAJI.**

Katika kipindi cha awamu ya sita uboreshaji wa huduma katika Sekta ya Maji umeimarika kwa kiwango kikubwa ambapo Jumla ya kiasi cha Tshs. bil. 50,927,124,011.00 kilipokelewa na kuwezesha kuboresha miundombinu ya maji katika miji ya Rujewa, Ubaruku, Imalilo Songwe na Igava. Hii ikiambatna na Sera ya Kumtua Mama ndoo kichwani.

Pia katika kuhakikisha mpango wa maji vijijini jumla ya Tshs. bil. 20,168,573,502.99 ilitumika katika kuboresha baadhi ya miradi iliyochakaa na kuanzisha miradi mipya, baadhi ya sehemu hizo ni uborehshaji wa mradi wa maji Chimala kwenye vijiji sita, upanuzi wa mradi wa maji kijiji cha Mkunywa, Upanuzi mradi wa maji kata ya Itamboleo kwenye vijiji vinne, upanuzi na ukarabati wa mradi wa maji Ilongo katika vijiji vinne, Mradi wa maji Luduga Mawindi awamu ya tatu na nne kwenye vijiji sita, mradi wa maji kibaoni, ujenzi wa mradi wa maji kwenye vijiji viwili Mwakaganga na Majengo.



SHULE YA MSINGI JAMHURI



MRADI WA UMWAGILIAJI




# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA:

## MWAKA 2022/2023 YAFANIKIWA KUONGEZA UKUSANYAJI MAPATO YA NDANI


JOSEPHINE KEENJA MANASE - MKUU WA WILAYA YA KYELA


SABRINA HUMOUD RUHWEY- KATIBU TAWALA KYELA

**Na KOKU DAVID-**
*MBEYA.*

**1. HISTORIA FUPI YA WILAYA.**
Wilaya ya Kyela ilianzishwa Mwaka 1972 baada ya kugawanywa Wilaya ya Rungwe ambayo toka mwaka 1961 – 1972 Kyela ilikuwa ni sehemu ya Wilaya hiyo.

**2. MAHALI WILAYA ILIPO.**
Wilaya ya Kyela ni moja kati ya Wilaya 5 za Mkoa wa Mbeya na ipo Kusini mwa Mkoa wa Mbeya. Kwa upande wa Mashariki Wilaya inapakana na Wilaya za Makete na Ludewa zote ni za Mkoa wa Njombe, kwa upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Ileje, upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya ya Rungwe na upande wa Kusini inapakana na Jamhuri ya Malawi.

**3. ENEO.**
Wilaya ina eneo la Kilometa za Mraba 1,322 kati ya hizo 450 sawa na 34.03% ni eneo la maji likijumuisha Ziwa Nyasa na mito mikubwa ya Mbaka, Lufilyu, Kiwira na Songwe pamoja na vijito. Eneo lililobaki la kilometa za mraba 872 ni ardhi kavu. Eneo linalotumika kwa shughuli za kilimo ni kilometa za mraba 481.28, sawa na 36.4% ya km za mraba, makazi yanachukua km za mraba 308.8 0 sawa na 23.3% ya eneo lote eneo lililobaki la Kilometa za mraba 81.92 ni msitu na mbuga za wazi.

**4. UTAWALA.**
Wilaya ya Kyela imegawanyika katika Tarafa 2 ambazo ni Unyakyusa na Ntebela. Aidha, Wilaya ina jumla ya Kata 33, vijiji 93 na vitongoji 407 ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mji Mdogo ambayo ilianzishwa mwaka 2008.

**5. IDADI YA WATU.**
Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Wilaya ya Kyela ilikuwa na jumla ya watu 266,426; wanaume ni 126,235 na wanawake ni 140,191, wastani wa watu kwa kaya ni 3.7 wanaojishughulisha na kilimo, biashara ufugaji na uvuvi.

**6. HALI YA UTUMISHI KATIKA WILAYA.**
Halmashauri ya Wilaya ya Kyela hadi sasa ina jumla ya watumishi 2,402

**7. SEKTA YA FEDHA NA BIASHARA.**
Halmashauri imeendelea kuongeza wigo wa Makusanyo ya Mapato ya Ndani kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023 kama inavyoonesha kwenye jedwali namba 1.
Jedwali Na: 1. Hali ya mapato ya Halmashauri kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023

| MWAKA | MAKISIO | MAPATO HALISI | % |
|---|---|---|---|
| 2019/2020 | 4,230,711,000.00 | 3,439,597,667.22 | 81 |
| 2020/2021 | 3,621,067,000.00 | 3,771,874,644.00 | 104 |
| 2021/2022 | 3,883,914,000.00 | 3,932,985,577.00 | 101 |
| 2022/2023 | 4,681,366,320.00 | 5,003,013,553.00 | 107 |

Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kuanzia mwaka 2019/2020 hadi mwaka 2022/2023 ilipata hati zifuatazo:-
Jedwali Na: 2. Hati zilizotolewa kwa halmashauri kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023

| MWAKA | HATI ILIYOTOLEWA |
|---|---|
| 2019/2020 | Safi |
| 2020/2021 | Safi |
| 2021/2022 | Safi |
| 2022/2023 | Safi |

**8. SEKTA YA AFYA.**
Wilaya ya Kyela ina jumla ya vituo 59 vya kutolea huduma za Afya, kati ya hivyo Hospitali 3, Vituo vya Afya 2, Zahanati 50 na kliniki za uzazi wa mama na mtoto 2. Kati ya vituo hivi, 35 vinamilikiwa na Serikali, 4 vya mashirika ya dini, 19 vya watu binafsi na 1 shirika la umma (Kiwira Coal Mine). Vituo hivi vinahudumia wananchi wapatao 266,426 ambapo 90% wanapata huduma ndani ya umbali wa kilomita 5.
Halmashauri imeendelea kutoa huduma za Afya kwa kutekeleza Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri na kwamba imeboresha huduma za Afya katika vituo vyote vya kutolea huduma vya Serikali na vile vya mashirika ya dini na binafsi kwa kuimarisha mpango wa ushirikiano na watoa huduma binafsi (Public Private Partnership - PPP).
Aidha, Halmashauri imeingia mkataba wa huduma "Service Agreement" na Hospitali ya Kilutheri ya Matema ili huduma za Afya ya uzazi na mtoto zitolewe bure. Katika mkataba huo Hospitali hiyo imekuwa ikipatiwa na Halmashauri rasilimali fedha, rasilimali watu, dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kuwahudumia walengwa.

**SEKTA YA ELIMU.**
**9. ELIMU MSINGI.**
Wilaya ya Kyela ina jumla ya Shule za Msingi 116 kati ya hizo 109 za Serikali na 7 sio za Serikali. Shule za Serikali zina jumla ya wanafunzi 58,088 kuanzia darasa la Awali – VII, wakiwemo wavulana 29,216 na wasichana 28,868 Shule hizi zina darasa I – VII, wanaotumia vyumba 1087 vya madarasa kati ya 1,337 vinavyohitajika. Shule hizi zina madawati 16,816 kati madawati 16,865 yanayohitajika, nyumba za walimu zipo 184 kati ya 1,337 zinazohitajika na matundu ya vyoo 1,408 kati 2,431 yanayohitajika.

**10. ELIMU YA SEKONDARI**
Wilaya ina jumla ya Shule za Sekondari 33 kati ya hizo 27 ni za Serikali na 6 sio za serikali. Shule za serikali zina Wanafunzi wapatao 17,965 kati ya hao wasichana ni 9,229 na wavulana ni 8,737. na shule zisizo za serikali zina jumla ya wanafunzi 690 Wavulana 267 na Wasichana 423.
Jumla ya wanafunzi wa shule za serikali na sisizo za serikari ni 18655 wavulana 9004 na wasichana 9651.
Halmashauri ina walimu 735 kati yao wakiume 512 na wakike 223.Aidha, walimu wa masomo ya sayansi ni 181 na sanaa ni 554 hata hivyo Halmashauri ina upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi 111.


KATULE GODFREY KINGAMKONO - MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA


FROLAH ANGELO LUHALA - MKURUGENZI HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA


Jengo la mama na mtoto Hospitali ya Wilaya ya Kyela



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Juma Zuberi Homera alipokagumradi wa umwagiliaji uliopo Kata ya Makwale wilayani Kyela.




Shule ya chekechea Kilambo Kata ya Njisi wilayani Kyela

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA:

## MWAKA 2022/2023 YAFANIKIWA KUONGEZA UKUSANYAJI MAPATO YA NDANI

**11. SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII.**

Idara ya Maendeleo ya Jamii inatekeleza shughuli mbalimbali za uwezeshaji wa Jamii kiuchumi na kijamii pamoja na uhamasishaji wa ushiriki wa wao katika utekelezaji wa shughuli za Maendeleo. Aidha, Idara ina jukumu la kuiwezesha kutambua na kutumia fursa zilizopo katika jamii husika, ili jamii ipate kuwa na uchumi wa kujitegemea.

**12. UIMARISHAJI WA VIKUNDI VYA UZALISHAJI MALI VYA WANAWAKE NA VIJANA.**

Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii inatekeleza jukumu madhubuti la kuhamasisha na kuwezesha jamii kujiunga katika vikundi kwa hiari, na kuviendeleza. ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa kwaka 2022/2023 imetoa mkopo wenye thamani ya Tshs. milioni 93,000,000 kwa vikundi 9,Vijana 3 na watu wenye ulemavu 3 na wanawake 3.

**13. SEKTA YA UJENZI.**

Wilaya ya Kyela imeunganishwa na mtandao wa barabara wenye jumla ya Km 662.07, kwa mchanganuo ufuatao; barabara za Kitaifa Km 45.2, Barabara za Kimkoa Km 102.28, barabara za Kiwilaya Km 226.79, Barabara za mjini Km 177.36 na Barabara za vijijini Km 110.32.

Barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) ni barabara za Kiwilaya, za Mjini na za Vijijini ambazo zina jumla ya km 514.59. Barabara za lami ni Km 5.3, za changarawe Km 75.7 na za udongo Km 433.59. Barabara nyingi zipo kwenye hali ya kuridhisha na zinapitika.

**14. SEKTA YA KILIMO.**

Halmashuri ya Wilaya ya Kyela ina ukubwa wa km za mraba 1,322, ambapo eneo linalofaa kwa shughuli za kilimo ni hekta 55,000. Kati ya hekta hizo, Hekta 12,720 zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, kwa msimu wa 2022/2023 zililimwa jumla ya hekta 52,009.8 Aidha, kwa msimu wa kilimo 2023/2024 Wilaya inatarajia kulima jumla ya hekta 52,500.50 za mazao mbalimbali.

Mazao makuu ya chakula yanayolimwa Wilayani Kyela ni Mpunga, Ndizi, Mihogo, Mahindi, Viazi vitamu na mazao ya biashara ni kakao, Mawese, Korosho.

Halmashauri imeendelea kusimamia upatikanaji wa mbolea kwa njia ya ruzuku ambapo kwa msimu wa kilimo 2022/2023 ilisajili wakulima 23,897 sawa na 71.69% ya lengo la kusajili wakulima 33,250 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea kwa mwaka 2022/2023. Aidha matumizi ya mbolea kupitia mfumo wa ruzuku yamefikia tani 1,569.7 ambayo ni sawa na ongezeko la matumizi ya mbolea ya tani 1,063 ukilinganisha na matumizi ya mbolea ya tani 506.7 katika msimu uliopita wa 2021/2022.

**15. SEKTA YA USHIRIKA.**

Katika kuboresha Ushirika Wilaya imesajiri Vyama vya Ushirika 47. Ikiwa chama kikuu kimoja (1), Vyama vya msingi 37 ambapo vyama vya ushirika wa mazao (AMCOS) na vyama vya ushirika vya aina nyingine 3. Aidha Wilaya imeendelea kusimamia mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani kwa zao la Kakao ambapo katika msimu wa 2022/2023 jumla tani 8,266,660 sawa na tani 8,266.66 kwa wastani wa shilingi 4,869 ambapo jumla ya Tshs. bil. 39,202,547,320.00 zimelipwa kwa wakulima na Tshs. bil. 1,041,599,160.00 zililipwa kama ushuru kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

**16. SEKTA YA MIFUGO.**

Wilaya ina jumla ya ngo'mbe 44,338 kati ya hao ngo'mbe 41,257 ni wa asili na ngo'mbe 3,081 ni wa maziwa. Aidha, kuna nguruwe 32,911, mbuzi wa asili 2,017, mbuzi wa maziwa 183, kondoo 487 na kuku wa asili 708,996, kuku wa kisasa 140,139, mbwa 5,429, bata 6,325, punda 8, kanga 1,407, bata mzinga 79, sungura 623, simbilisi 2,618, paka 5,861 na njiwa 416.

**17. MIUNDOMBINU YA MIFUGO NA RASILIMALI ZA IDARA YA MIFUGO NA UVUVI.**

Wilaya ina jumla ya majosho 12 ya kuogesha ng'ombe na kwamba kati ya hayo 8 yanafanyakazi na 4 ni mabovu ambayo yapo katika mpango wa kukarabatiwa. Mpango huu ni katika jitihada za kuzuia magonjwa yaenezwayo na kupe hapa wilayani. Pia idara ina machinjio kubwa 3 za ng'ombe, machinjio ndogo 12 za nguruwe, mnada 1, pikipiki 2 ambazo ni nzima, laptop 6, Desktop 6 na jokofu 9.



Mradi wa Michikichi



Shule ya msingi Kilambo Kata ya Njisi Wilayani Kyela



Bwawa la ufugaji Samaki



Mashine ya utotoleshaji wa vifaranga vya Samaki

## WIZARA YA MAJI
## MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MBEYA

# ZAIDI YA BILIONI 200/= ZATUMIKA KUBORESHA HUDUMA YA MAJISAFI MKOANI MBEYA



Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji kutoka chanzo cha mto Ilunga ukiendelea

***Katika kipindi cha Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mbeya-UWSA chini ya Wizara ya Maji imepanga kutumia kiasi cha Tshs. bil. 202 kutekeleza jumla ya miradi ya maji 12 ya kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Mbeya, Mji wa Mbalizi, Mji wa Tukuyu, Mji wa Kasumulu, Wilaya ya Chunya, Kyela na Wilaya ya Mbarali.***

**Na KOKU DAVID-** *MBEYA.*

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya(MBEYA-UWSA) ilianzishwa mwezi Januari, 1998 kwa sheria ya Maji sura 281 ya mwaka 1998, iliyofanyiwa marekebisho na kufutwa kwa sheria Na.5 ya Huduma za Majisafi na Mazingira ya mwaka 2019.

Mamlaka hii ipo katika Daraja A na hii ina maana kuwa Mbeya-UWSA ina uwezo wa kugharamia shughuli zote za uendeshaji, matengenezo na kuchangia uwekezaji kwenye upanuzi wa miundombinu ya huduma.

Aidha, Mamlaka ilianzishwa kwa misingi ya kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa misingi ya kibiashara, msisitizo ukiwa ni kudhibiti matumizi ya maji kwa kufunga dira (mita), na kuhamasisha wateja kutumia maji kwa uangalifu ili huduma iwafikie wakazi wengi zaidi na kuifanya huduma iwe endelevu.

Kwa kuzingatia misingi hiyo, Mamlaka inatekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi ambayo imewezesha wananchi kupata nafasi ya kufanya shughuli zingine za kimaendeleo kwani huduma ya maji ni kichocheo cha usalama wa afya, ustaarabu na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Miradi hii inatekelezwa ili kukidhi mahitaji ya wananchi na kufikia lengo la upatikanaji wa huduma ya maji Mbeya mjini kwa asilimia 95 na vijijini kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2025. Aidha, kwa sasa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Jiji la Mbeya na mji wa Mbalizi ni asilimia 80 za mahitaji hivyo Serikali imejipanga kuboresha huduma kwa kubuni na kutekeleza miradi ya maji ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

Katika kipindi cha Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mbeya-UWSA chini ya Wizara ya Maji imepanga kutumia kiasi cha Tshs. bil. 202 kutekeleza jumla ya miradi ya maji 12 ya kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Mbeya, Mji wa Mbalizi, Mji wa Tukuyu, Mji wa Kasumulu, Wilaya ya Chunya, Kyela na Wilaya ya Mbarali.

Miradi hiyo ni mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi katika Jiji la Mbeya kutoka chanzo cha mto Kiwira, Mradi wa maji kutoka mto Ilunga, Mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Kata za Mwasenkwa na Iganzo, Mradi wa maji toka mto Halinji, Mradi wa chanzo cha Mto Simba, Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Tukuyu, Kyela – Kasumulu, Mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi Kata ya Ipinda, Ujenzi wa mradi wa maji kutoka chanzo cha Mto Mwega, Mradi wa maji Chunya wa Matokeo ya haraka (Quick Wins), Mradi wa kuboresha huduma ya maji chini ya Programu ya Miji 28, Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Mbarali kupitia Programu ya Miji 28.

### MRADI WA KUBORESHA HUDUMA YA MAJISAFI KUTOKA CHANZO CHA MTO KIWIRA

Mradi huu ni wa kimkakati wa kuboresha huduma ya Majisafi katika Jiji la Mbeya na mji wa Mbalizi ili kukidhi mahitaji ya wananchi kwani kwa sasa Mbeya-UWSA inazalisha maji lita milioni 66.5 kwa siku ingali uhitaji wa maji kwa Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi ni lita ni lita milioni 90 kwa siku. Utekelezaji wa mradi huu utamaliza changamoto ya upatikanaji wa maji kwani unatarajiwa kuzalisha maji lita milioni 117 kwa siku na kufikia uzalishaji wa lita milioni 187 kwa siku, hivyo kukidhi kiasi cha maji kinachohitajika kutosheleza wananchi 1,452,000 hadi kufikia mwaka 2045.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji imetoa kiasi cha Tshs. bil. 119 ili kutekeleza mradi huo kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwezi Machi 2023 hadi Machi 2025; kwa kutumia Mhandisi Mshauri Lahmeyer Consult Engineering Co. Ltd na Mkandarasi China Railway Engineering Co.Ltd.

Kazi zitakazo fanyika ni Ujenzi wa chanzo cha maji katika Mto Kiwira, Uchimbaji na ulazaji wa bomba kuu la chuma lenye kipenyo cha mita1.4 kwa umbali wa km 26.3 la mseleleko kutoka chanzo hadi Sistila, Ujenzi wa chujio la kutibu maji eneo la Nsenga Kata ya Swaya, Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji yaliyotibiwa lenye uwezo wa Lita Milioni 5 eneo la Sistila, Uchimbaji na ulazaji wa bomba kuu la mseleleko kutoka eneo la chujio hadi New Forest lenye kipenyo cha mita 1.2 kwa umbali wa km 11 na Ujenzi wa tenki la kuhifadhi maji eneo la New Forest lenye uwezo wa Lita Milioni 5.

### MRADI WA MAJI WA ILUNGA

Kwa kutumia wataalamu wa ndani Mbeya- UWSA imebuni



Usafishaji wa eneo la chanzo cha Maji Mto Kiwira kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika chanzo hicho.

# ZAIDI YA BILIONI 200/= ZATUMIKA KUBORESHA HUDUMA YA MAJISAFI MKOANI MBEYA

na kutekeleza mradi wa maji wa Ilunga ambao umelenga kuhudumia wananchi 110,000 wa maeneo ya Iwambi, Sistila, Ihombe, Itimba, Idugumbi, Songwe na Mbalizi.

Hadi kukamilika kwake mradi huu utagharimu kiasi cha Tshs. bil. 4.8 kwa kazi za Ujenzi wa banio, Uchimbaji na ulazaji wa bomba kuu HDPE 10" kwa umbali wa km 11.5, Ujenzi wa chujio la kutibu maji, Uchimbaji na ulazaji wa bomba HDPE 4" kuelekea Itimba km 11, Uchimbaji na ulazaji wa bomba HDPE 6" kuelekea Sistila na Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye uwezo wa kuhifadhi maji yaliyotibiwa lita milioni 2.

Utekelezaji wa mradi huu ni wa miaka miwili kuanzia mwaka 2021 hadi Novemba 2023 mradi umefikia asilimia 82 na tayari wananchi wameanza kunufaika na huduma ya maji kutoka chanzo cha maji kutoka mto Ilunga. Shughuli za mradi zilizobaki ni ujenzi wa chujio la kutibu maji na tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita milioni 2.

> Miradi hiyo ni Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Tukuyu, Kyela – Kasumulu , Mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi Kata ya Ipinda , Ujenzi wa mradi wa maji kutoka chanzo cha Mto Mwega, Mradi wa maji Chunya wa Matokeo ya haraka (Quick Wins), Mradi wa kuboresha huduma ya maji chini ya Programu ya Miji 28 na Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Mbarali kupitia Programu ya Miji 28, miradi hii itatekelezwa kwa gharama ya Tshs. bil. 81.1 ambazo zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji.

### MRADI WA KUBORESHA HUDUMA YA MAJISAFI KATIKA KATA ZA MWASENKWA NA IGANZO

Serikali kupitia Mbeya-UWSA inatekeleza mradi huu kwa Tshs. bil. 5.2 kwa vipengele (LOTS) viwili chini ya wakandarasi wawili ambao ni DMUKE Engineering Co Ltd anayejenga chujio la kutibu maji na ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji yaliyotibiwa lita milioni 1.5 na GOPA Construction Co.Ltd anayejenga banio mbili za maji katika vyanzo vya Hanzya na Hasara, uchimbaji na ulazaji wa bomba kuu aina ya HDPE 4" kutoka vyanzo hadi chujio kwa umbali wa km 3.8.

Mradi utazalisha maji lita milioni 2.6 kwa siku na kunufaisha wananchi 42,000 wa maeneo ya Kata ya Iganzo(Iganzo, Mwambenja na Nkuyu), Kata ya Mwasenkwa( Luala, Mwazumbo , Ilembo na Mengo) na baadhi ya maeneo ya kata ya Ilemi. Mradi huu umeanza kutekelezwa mwezi April mwaka 2023 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Januari 2024.



Ujenzi wa banio katika Mto Mambwe- Mradi wa kuboresha huduma za maji Kyela Mjini Wilaya ya Kyela.

### MIRADI YA KUBORESHA HUDUMA YA MAJISAFI TOKA MTO SIMBA NA HALINJI

Katika mwaka huu wa fedha 2023/2024, Mbeya-UWSA imesanifu mradi kuboresha huduma ya maji Halinji ambao utaboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya Uyole na mradi wa maji toka chanzo cha mto Simba ambao utahudumia wananchi wa maeneo ya Mwansanga, Shewa na Ituha.

Usanifu wa miradi hii umekamilika na itatekelezwa kwa kutumia wataalamu wa ndani pamoja na Wakandarasi kwa gharama ya Tshs. bil. 1.3.

### USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI MIRADI KATIKA MAMLAKA ZA CHUNYA ,KYELA NA RUNGWE

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya imepewa dhamana ya kusimamia uzalishaji na usambazaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi, pia imepewa jukumu na Serikali kupitia Wizara ya Maji, kusimamia baadhi ya Mamlaka ndogo katika wilaya ya Chunya, Kyela na mji wa Kasumulu, pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji katika wilaya za Mbarali, Kyela.

Miradi hiyo ni Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Tukuyu, Kyela – Kasumulu , Mradi wa kuboresha huduma ya Majisafi Kata ya Ipinda , Ujenzi wa mradi wa maji kutoka chanzo cha Mto Mwega, Mradi wa maji Chunya wa Matokeo ya haraka (Quick Wins), Mradi wa kuboresha huduma ya maji chini ya Programu ya Miji 28 na Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Wilaya ya Mbarali kupitia Programu ya Miji 28, miradi hii itatekelezwa kwa gharama ya Tshs. bil. 81.1 ambazo zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya inamshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kutoa fedha za kutekeleza miradi hii. Aidha Mbeya-UWSA inaishukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kuwezesha hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi hii. Kwa namna ya pekee Mbeya-UWSA inatoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kwa mchango wake katika kusimamia utekelezaji wa Ilani kupitia miradi ya kuboresha huduma ya majisafi.



Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita milioni 1.5 katika mradi wa kuboresha huduma za Maji Tukuyu Wilaya ya Rungwe.




# MBEYA DC: Tumefanikiwa kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato ya ndani



BENO MALISA - MKUU WA WILAYA YA MBEYA



AZIZI FAKIRI MOHAMED - KATIBU TAWALA WILAYA YA MBEYA

**Na KOKU DAVID-**
*MBEYA.*

**HISTORIA FUPI YA WILAYA.**
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilianzishwa Mwaka 1984 kama Halmashauri ya Wilaya baada ya kuanza kufanya kazi kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 (1982).

**MAHALI ILIPO NA MIPAKA YAKE**
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ipo kati ya Latitude 7° na 9° Kusini mwa Ikweta na Longitude 33° na 35° Mashariki mwa Greenwich. Wilaya inapakana na Wilaya ya Mbarali kwa upande wa Mashariki, Rungwe na Ileje upande wa kusini, Magharibi imepakana na Mbozi na Kaskazini Wilaya ya Chunya.

**ENEO.**
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina eneo la Ukubwa wa Kilometa za Mraba 2,432 ambazo ni sawa na hekta 243,200. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 216,400 sawa na asilimia 88. Kati ya hekta 216,400 ni hekta 98,710 zinazotumika kwa shughuli za kilimo. Halmashauri ina jumla ya hekta 4,335 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kati ya hizo ni hekta 2,492 zinazotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Hii inasababishwa na miundombinu duni ya kilimo cha umwagiliaji iliyopo.

**UTAWALA.**
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina jumla ya Tarafa 3, Kata 28, vijiji 140 na Vitongoji 918. Mnano mwaka 2014 Mamlaka ya mji mdogo Mbalizi ulianzishwa.

**IDADI YA WATU.**
Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina jumla ya watu 371,259; wanaume ni 173,158 na wanawake ni 198,101,wastani wa watu kwa kaya ni 3.7 wanaojishughulisha na kilimo, biashara na ufugaji.

**HALI YA UTUMISHI KATIKA WILAYA.**
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya hadi sasa ina jumla ya watumishi 3,563

**SEKTA YA FEDHA NA UHASIBU.**
Hali ya Wilaya ya Mbeya imeendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuongeza wigo wa ukusanyaji, ambapo mapato ya Halmashauri yameongezeka kutoka asilimia 104 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia asilimia 107 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 1 hapa chini.

Jedwali Na. 1: hali ya kukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2022.2023

| Mwaka | Makisio kwa mwaka | Maakusanyo kwa mwaka | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 3,888,212,000.00 | 4,061,865,273.00 | 104 |
| 2021/2022 | 4,372,505,400.00 | 5,291,253,639.00 | 110 |
| 2022/2023 | 4,810,300,000.00. | 5,158,921,688.57 | 107 |
| 2023/2024 hadi Septemba 30 | 4,978,660,000.00 | 1,724,915,825.58 | 35 |
| JUMLA KUU | 13,239,377,400.00 | 16,236,956,426.15 | |

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuanzia mwaka 2020/2021 hadi mwaka 2022/2023 ilipata hati zifuatazo:-

Jedwali Na: 2. Hati zilizotolewa kwa halmashauri kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023

| MWAKA | HATI ILIYOTOLEWA |
|---|---|
| 2020/2021 | Safi |
| 2021/2022 | Safi |
| 2022/2023 | Safi |

**SEKTA YA AFYA.**
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina vituo 86 vya kutolea huduma za Afya, kati ya hivyo Hospitali zipo 3 ambazo 1 inamilikiwa na Serikali, nyingine inamilikiwa na Taasisi wakati nyingine inamilikiwa na shirika la dini.

Aidha, kuna Zahanati 77 na Vituo vya Afya 6 ambapo kati ya vituo hivyo 5 vinamilikiwa na Serikali na 1 kinamilikiwa na mtu binafsi. Vituo hivi vinahudumia wananchi wapatao 371,259 ambapo asilimia 90 wanapata huduma ndani ya umbali wa kilomita 5.

Aidha, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni miongoni mwa Hospitali zilizopata fedha toka Serikali Kuu kwa ajili ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka Ibara ya 83(g) ambayo inaelekeza kila Wilaya kuwa na hospitali ya Wilaya iliyokamilika na inayotoa huduma kwa wananchi.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya katika utekelezaji wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya hadi kufikia Juni 30, 2023 imepokea na imetumia kiasi cha Shilingi 3,139,000,000.00, ambapo Tshs. bil. 2,700,000,000.00 ni fedha toka Serikali Kuu, Tshs. milioni 250,000,000.00 ni fedha za Wahisani (UVICO-19), Tshs. milioni 99,000,000.00 ni mapato ya ndani ya Halmashauri na Tshs. milioni 90,000,000.00 ni nguvu za wananchi.

Aidha, Hospitali hii ilianza kutoa huduma kuanzia mwezi Mei 1, 2020 ambapo ilikuwa ni kituo Maalum cha Mkoa kwa ajili ya wagonjwa wa UVIKO-19 hadi ilipofika mwezi Julai 2020 ilianza huduma za wagonjwa wa nje baada ya kufunga huduma za UVIKO-19. kwa sasa Hospitali inatoa huduma za wagonjwa wa nje na huduma ya Mama na mtoto.

**SEKTA YA ELIMU.**
**ELIMU YA AWALI NA MSINGI.**
Wilaya ya Mbeya ina jumla ya Shule za Msingi 173 kati ya hizo 163 ni za Serikali na 10 zinamilikiwa na watu binafsi. Shule za Serikali zina jumla ya wanafunzi 87,353 kuanzia darasa la Awali – VII, wakiwemo wavulana 43,558 na wasichana 43,795 na kwamba shule hizi zina darasa I – VII. Shule hizi zina madawati 22,480 kati madawati 24,996 yanayohitajika, nyumba za walimu zipo 501 kati ya 1951 zinazohitajika na matundu ya vyoo 2384 kati 3802 yanayohitajika.

Aidha katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilipokea jumla ya Tshs. bil. 1,451,100,000.00 ikiwa ni fedha za Wahisani (BOOST) ambapo fedha hizi zimetumika kujenga madarasa 45, matundu ya vyoo 69 na majengo 2 ya Utawala katika shule 7 za awali na msingi. Pia kati ya shule hizi 7 shule 2 ni shule mpya ambazo zimegharimu Tshs. bil. 1,077,000,000.00 ambapo ujenzi wa miundombinu katika shule hizo umekamilika.

**ELIMU YA SEKONDARI**
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina jumla ya Shule za Sekondari 61 kati ya hizo 37 ni za Serikali na 24 zinamilikiwa na watu binafsi. Shule za Serikali zina wanafunzi wapatao 19,650 kati ya hao wasichana ni 11,241 na wavulana ni 8,408, na shule zisizo za serikali zina jumla ya wanafunzi 7,240 Wavulana 3,718 na Wasichana 3,522.

Shule za Serikali zina vyumba 448 vya madarasa kati ya 449 vinavyohitajika. Shule hizi zina madawati 19,328 kati madawati 19478 yanayohitajika, nyumba za walimu zipo 117 kati ya 856 zinavyohitajika na matundu ya vyoo 740 kati 860 yanayohitajika. Halmashauri ina walimu 856 kati yao wakiume 580 na wakike 276. Aidha Halmashauri ina upungufu wa walimu 15.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imefanikiwa kujenga shule 1 ya wasichana Galijembe ambayo hadi Novemba 2023 imetumia jumla ya Tshs. bil. 1,083,146,669.00 ambapo kati ya fedha hizo Tshs. milioni 369,225,000.00 ni za Serikali Kuu, huku Tshs. milioni 60,0092,369.00 ni mapato ya ndani ya Halmashauri, na Tshs. milioni 24,075,200.00 ni michango ya wadau mbalimbali wakati Tshs. milioni 89,754,100.00 ni michango ya wananchi.

Kwa sasa shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 329 kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne. Aidha, Kwa mwaka 2022 walisajiliwa wanafunzi 50 kufanya mtihani wa Taifa kidato cha nne, wanafunzi 47 walichaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha tano katika shule mbalimbali za Serikali wakati wanafunzi 3 walichaguliwa kujiunga na vyuo mbalimbali vya serikali.

**SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII.**
Idara ya Maendeleo ya Jamii inatekeleza shughuli mbalimbali za uwezeshaji wa Jamii kiuchumi na kijamii



MWALINGO M KISEMBA - MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA



STEPHEN E. KATEMBA - MKURUGENZI HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA





Jengo la shule mpya ya msingi Muungano


Jengo la wagojwa mahututi (ICU)


Shule mpya ya msingi Muungano


Choo

# Tumefanikiwa kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato ya ndani

pamoja na uhamasishaji wa ushiriki wao katika utekelezaji wa shughuli za Maendeleo. Aidha, Idara ina jukumu la kuwezesha, kutambua na kutumia fursa zilizopo katika jamii husika, ili jamii ipate kuwa na uchumi wa kujitegemea.

**UIMARISHAJI WA VIKUNDI VYA UZALISHAJI MALI VYA WANAWAKE NA VIJANA.**

Halmashauri kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamii inatekeleza jukumu madhubuti la kuhamasisha na kuwezesha jamii kujiunga katika vikundi kwa hiari, na kuviendeleza, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2020/2021 hadi 2022/2023 imetoa mkopo wenye thamani ya Tshs. bil. 2,169,400,000 kwa vikundi 117 Vijana 53 na watu wenye ulemavu 5 na wanawake 59. Kiasi kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya kukopesha makundi hayo ni Tshs. bil. 1,520,722,476.80

Jedwali Na. 3: Hali ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu.

MAFANIKIO YA MAMA MIKOPO YA 10% KUANZIA MWAKA 2020/2021 HADI 2023/2024

| MWAKA | KIASI KILICHOTENGWA | KIASI KILICHOTOLEWA KWENYE VIKUNDI | IDADI YA VIKUNDI |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 348,724,026.80 | 839,000,000 | 54 |
| 2021/2022 | 360,962,400 | 657,900,000 | 37 |
| 2022/2023 | 397,100,000 | 672,500,000 | 26 |
| 2023/2024 | 413,936,050 | 0 | 0 |
| JUMLA | 1,520,722,476.80 | 2,169,400,000 | 117 |

SEKTA YA UJENZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina mtandao wa barabara zenye urefu wa jumla km 1,488.53 Kati ya hizo barabara za Mkoa na barabara kuu zina urefu wa Km 376.2, na barabara za Wilaya na Vijiji zina urefu wa Km 1,112.33. Aidha, Wilaya inapitiwa na Reli ya Tazara kwa urefu wa km 46 vile vile kuna uwanja wa ndege wa Kimataifa eneo la Songwe. Kwa wastani asilimia 65 za barabara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya zinapitika.

**SEKTA YA KILIMO UVUVI NA MIFUGO**

**KILIMO**

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina eneo la Ukubwa wa Kilometa za Mraba 2,432 ambazo ni sawa na hekta 243,200. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 216,400 sawa na asilimia 88.

Kati ya hekta 216,400 ni hekta 98,710 zinazotumika kwa shughuli za kilimo. Halmashauri ina jumla ya hekta 4,335 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kati ya hizo ni hekta 2,492 zinazotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Hii inasababishwa na miundombinu duni ya kilimo cha umwagiliaji iliyopo.

Halmashauri imeendelea kusimamia upatikanaji wa mbolea kwa njia ya ruzuku ambapo kwa msimu wa kilimo 2022/2023 ilisajili wakulima 91357 sawa na asilimia 109 ya lengo la kusajili wakulima 90,500 kwa ajili ya Ruzuku ya mbolea kwa mwaka 2022/2023. Aidha matumizi ya mbolea kupitia mfumo wa ruzuku yamefikia tani 38,627 ambayo ni sawa na ongezeko la matumizi ya mbolea ya tani 31,259 ukilinganisha na matumizi ya mbolea ya tani 3,295 katika msimu uliopita wa 2021/2022.

**MIFUGO.**

**IDADI YA MIFUGO**

Idadi ya mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa mwaka 2022/2023 ni kama inavyoonekana hapa chini.

Jedwali Na. 4: Aina ya mifugo

| NA | AINA YA MNYAMA | IDADI YA WANYAMA |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 71,463 |
| 2 | Mbuzi | 65,489 |
| 3 | Kondoo | 9,852 |
| 4 | Nguruwe | 20,942 |
| 5 | Kuku | 555,405 |
| 6 | Bata | 1,538 |
| 7 | Sungura | 361 |
| 8. | Kanga | 159 |
| 9. | Bata mzinga | 36 |
| 10. | Punda | 2,289 |
| 11. | Mbwa | 11,527 |
| 12. | Paka | 4,121 |
| | Jumla | 743,182 |

**MIUNDOMBINU YA MIFUGO NA RASILIMALI ZA MIFUGO**

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina jumla ya majosho 18 ya kuogeshea mifugo na kati ya hayo 8 yanafanyakazi na 4 ni mabovu ambayo yapo katika mpango wa kukarabatiwa. Mpango huu ni katika jitihada za kuzuia magonjwa yaenezwayo na kupe hapa wilayani. Pia idara ina machinjio kubwa 1 na ndogo 5 za ng'ombe,mbuzi na kondoo, machinjio 1 ya nguruwe, minada 2.

**UVUVI**

Halmashauri ya Willaya ya Mbeya kwa 2022/2023 ilikuwa na jumla ya wafugaji wa samaki 562, wenye mabwawa 811 yenye ukubwa wa mita za mraba 233,891 yenye uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 55.2 za samaki.

Pia halmashauri ina kituo kimoja binafsi cha kuzalisha vifaranga vya samaki chenye uwezo wa kuzalisha wastani wa vifaranga 40,000 kwa juma ila kwa sasa kinazalisha wastani wa vifaranga 10,000 kwa juma.

SEKTA YA USHIRIKA.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina jumla ya vyama vya ushirika 68 vilivyosajiliwa. Jedwali hapa chini linaoneshwa kwa muhtasari maendeleo ya vyama vya ushirika:

Jedwali Na. 5: Hali ya vyama vya Ushirika ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

| NA | AINA YA VYAMA VYA USHIRIKA | IDADI | WANACHAMA | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ME | KE | |
| 1. | Ushirika wa Mazao (AMCOS) wenye jumla ya Hisa Tshs. 155,987,206.00 | 38 | 3978 | 805 | 4803 |
| 2. | Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) zenye jumla ya hisa Tshs. 1,011,359,994.00 Akiba Tshs. 3,370,637,667.00 na amana Tshs. 361,775,926.00 | 25 | 4388 | 2734 | 7584 |
| 3. | Ushirika wa aina nyingine vyenye jumla ya mtaji Tshs. 13,550,000.00 | 5 | 484 | 298 | 782 |



## HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA MBEYA

# Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya yajivunia kutoa huduma za kibingwa

**Na KOKU DAVID** - *Chunya*

Unapotembelea Mkoa wa Mbeya utakutana na zaidi ya hospitali 10, lakini moja ya hospitali inayotajwa zaidi na wananchi wa Mbeya ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya (MZRH) iliyo chini ya kilele cha mlima Loleza kutokana na ubora wa huduma za matibabu zinazotolewa na MZRH.

MZRH ni hospitali kubwa inayotoa huduma za matibabu katika mikoa saba ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Iringa, Njombe, Ruvuma, Songwe, Rukwa na Katavi). Pia inahudumia zaidi ya wananchi milioni 10 ndani na nje ya Jiji la Mbeya.

Uwepo wa hospitali hii katika Mkoa wa Mbeya umesaidia kusogeza huduma za matibabu karibu na wananchi jambo ambalo wakazi wa kanda ya Nyanda za Juu Kusini wanajivunia uwepo wa hospitali hii hasa kutokana na huduma za kibingwa zinapatikana ikiwa ni pamoja na uwepo wa wataalamu wabobezi katika huduma za afya.

Hivi sasa hospitali ina madaktari zaidi ya 108 katika fani mbalimbali na kwamba kati yao 56 ni madaktari bingwa, 5 ni madaktari Bingwa Wabobezi, Wafamasia wa 7, Wateknolojia Dawa 11, Wateknolojia maabara 25, Wauguzi 198 na Wasaidizi Afya 238.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Dkt. Godlove Mbwanji anaeleza gazeti Uhuru Kijani kuwa jitihada zilizofanywa na MZRH katika kuunga mkono azma ya Serikali kuelekea Tanzania ya Viwanda, ndani ya miaka 2 ya Serikali ya Awamu ya 6 inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia S. Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuboresha miundombinu ya hospitali ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za afya zinazotolewa.

Anasema hospitali imeboresha miundombinu kwa tengeneza gari maalum la kubebea wagonjwa ndani ya hospitali na kuondokana na huduma ya kutumia viti mwendo au vitanda vya kusukuma wagonjwa pindi wanapokuwa ndani ya hospitali kwaajili ya kupatiwa huduma.

"Yapo mafanikio mengi ambayo sisi kama hospitali tunajivunia, hii ni pamoja na kuanzishwa kwa kiwanda cha uzalishaji maji tiba ambacho kwa siku kiwanda hicho kinazalisha lita 120 zinazotumika ndani ya hospitali kwa asilimia 76 na tunakuwa na akiba ya kutosha.

"Lakini pia tunajivunia kuweza kutoa mafunzo ya udaktari katika ngazi ya shahada kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kwamba kwa sasa chuo kina takriban ya wanachuo 1,000," anasema Dkt Mbwanji.

Dkt. Mbwanji anasema kuwa hospitali kwa sasa inatoa huduma za kibingwa za upasuaji wa kawaida, upasuaji kwa njia ya vitundu (Laparascopic Surgery), upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu pamoja na usafishaji wa figo (haemodialysis).

Anaendelea kuzitaja huduma nyingine zinazopatikana katika hospitali hiyo kuwa ni pamoja na huduma za kibingwa za magonjwa ya ndani (Internal Medicine), Huduma za kibingwa na kibobezi za magonjwa ya moyo na mishipa ya damu (Cardiac diseases) pamoja na mfumo wa hewa (Pulmonology), matibabu ya figo (Renal/Nephlorogy), matibabu ya ngozi, matibabu ya damu (Haematology) na matibabu ya saratani (Cancer).

Anaongeza kuwa, sambamba na hiyo pia hospitali imefanikiwa kuanzisha maabara ya kisasa iliyopewa Ithibati ya kimataifa Accreditation (Immunohistochemistry, Serology na Haematology Hematology, Molecular biology, Parasitology, Bacteriology, TB, Blood Transfusion, Serology, Immunophenotyping (CD4 lab), Histopathology na Clinical chemistry) yenye uwezo wa kufanya vipimo katika ngazi ya kimataifa, lakini pia ina uwezo wa kupima magonjwa ya Ebola na mengine yanayofanana na hayo.

Anasema katika kipindi cha Serikali ya awamu ya sita, hospitali hiyo imeweza kupatiwa mashine mpya ya MRI yenye thamani ya kiasi cha Tshs bil. 3 pamoja na mashine 2 za digital x ray.

"Pamoja na hayo hospitali ina vifaa vya kisasa vya uchunguzi vya Radiolojia vya CT scan, Fluoroscopy, Digital X-Ray, Mammography ambavyo vinawawezesha madaktari kutoa tiba stahiki kwa wagonjwa na kwa wakati.

"Pia tumeboresha huduma kwa kutumia mfumo wa kieletroniki (eMedical) unaosaidia kudhibiti upotevu wa mapato hivyo kujiendesha kwa ufanisi. Tunao mfumo wa Nursing call ambapo mgonjwa akihitaji usaidizi wa muuguzi anabonyeza kitufe ambacho humuwezesha muuguzi kujua kuwa anahitajika kutoa msaada kwa mgonjwa yupi,"anasema Dkt Mbwanji.

Anasema pamoja na maboresho yote yaliyofanyika katika hospitali hiyo, Serikali imeweza kukamilisha ujenzi wa jengo la afya ya mama na mtoto lilogharimu kiasi cha Tshs. bil. 12.4 ambapo imejengwa wodi ya kisasa ya wazazi (vitanda 223) Meta ambayo ni sehemu ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na kwamba limeshaanza tumika. Pia serikali ilitoa kiasi cha Tshs. bil. 5 kwaajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba .

Mbali na hilo, Dkt Mbwanji anasema kuwa katika kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita wameweka mpango mkakati wa kuanzisha huduma za upasuaji wa moyo na mishipa ya damu na kwamba hadi sasa wataalamu wapo, ukarabati wa vyumba vya upasuaji unaendelea ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba unakaribia kumalizika.

Anasema mipango mingine ya baadaye ni kupeleka wataalamu kwenye mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili kuboresha huduma katika vitengo vya tiba na uchunguzi, pamoja na kupanua huduma za kibingwa na kibobezi kwenye maeneo mbalimbali ya hospitali. Aidha mipango hiyo ni pamoja na huduma za matibabu ya magonjwa ya saratani kwa njia ya mionzi na kuendelea kuboresha utoaji wa dawa za saratani na huduma za maabara.

"Hospitali yetu ilipata fursa ya kushiriki kwenye maonyesho ya Lusaka, Zambia ili kujitangaza kuhusiana na tiba za utalii na huduma zetu za matibabu. Kupitia ushiriki wetu kwenye maonyesho hayo, tulipata fursa ya kufikia watazamaji wengi na kuelezea jinsi tiba yetu ya utalii inavyoweza kusaidia katika afya na ustawi wa watu.

"Katika maonyesho yale tulipata nafasi ya kuweka banda letu ambako tuliweza kutoa habari na ufahamu kuhusu namna tiba ya utalii inavyoweza kutumika kutibu na kuzuia magonjwa mbalimbali, pia tulitoa maelezo kuhusu faida za mazoezi, lishe bora, tiba ya mimea, na njia nyingine za asili za matibabu ambazo tunazingatia katika hospitali yetu," anasema Dkt Mbwanji.

Anasema kuwa, pia walitoa maelezo kuhusu huduma zao za matibabu na vifaa vya kisasa ambavyo wanatumia kwa lengo la kutoa huduma bora na yenye ufanisi kwa wagonjwa wao na kwamba katika maonyesho yale waliambatana na timu ya wataalamu wao ambao walitoa ushauri na kujibu maswali ya wageni wote kwa ufanisi.

Anaongeza kuwa kushiriki kwao kwenye maonyesho hayo pia kuliwasaidia kujenga uhusiano na wadau wengine katika sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kupata fursa ya kubadilishana uzoefu na hospitali nyingine na taasisi za matibabu, lakini pia hata kushiriki katika majadiliano na wataalamu wengine hali ambayo ilisaidia kuimarisha uhusiano wao na kuwaongezea ufahamu katika eneo hilo.



Dkt. Godlove Mbwanji - Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, akizindua jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya (MZRH)



Jengo la mama na mtoto Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya



Mashine ya MRI


Atomic Absoption Spectrophotometer (AAS). Mtambo ambao hutumika kubaini kiasi cha dhahabu na madini mengine kwenye sampuli mbalimbali ikiwemo udongo na maji.

# MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI MBEYA

**Na KOKU DAVID-** *MBEYA*

Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni taasisi chini ya Wizara ya Afya na ilianzishwa mwaka 1895, enzi za Ukoloni wa Kijerumani. Ilitangazwa kuwa Mamlaka chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Na.8 ya mwaka 2016 mnamo tarehe 5 Aprili 2017.

Majukumu ya Mamlaka yamegawanyika katika maeneo makuu matatu ambayo ni:

a) Kufanya Uchunguzi wa Kimaabara wa Sampuli mbalimbali ikiwemo ubakaji, kupatikana na viungo vya binadamu, mauaji kwa kutumia sumu, biashara na matumizi ya dawa za kulevya na ujangili wa wanyama pori na uhalali wa mzazi kwa mtoto.

Sampuli nyingine ambazo zinafanyiwa uchunguzi ni za mazao ya kilimo na uvuvi, maji, bidhaa za chakula, mbolea na bidhaa za viwandani.

b) Kusimamia utekelezaji wa sheria tatu ikiwemo Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sheria Na.8 ya 2016. Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura 182 na Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Vinasaba vya Binadamu, Sura 73.

c) Kutoa Ushauri wa Kitaalamu kwa Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na uchunguzi wa kimaabara. Vilele kutoa ushahidi wa kitaalam mahakamani kwa kesi ambazo uchunguzi umefanyika kwenye maabara za Mamlaka.

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kanda ya Nyanda za Juu kusini Mbeya kwa kipindi cha miaka mitatu imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

**USAJILI NA UKAGUZI WA WATUMIAJI WA KEMIKALI.**

Katika kipindi cha mwezi Machi, 2021 hadi Oktoba 2023, ofisi iliweza kukagua na kusajili wadau 150 wanaojishughulisha na matumizi na biashara ya kemikali kwa mkoa wa Mbeya lengo ni kuthibiti matumizi mabaya yakemikali ili kulinda afya ya binadamu, wanyama na mazingira. Usajili wa wadau unasaidia kuwatambua pamoja na aina ya kemikali ambazo wanatumia ili kuepusha uchepushaji wa kemikali ambao unaweza kujitokeza na kupelekea kutumika katika kutengeneza dawa za kulevya au milipuko.

Mafunzo kwa watumiaji wa kemikali Ili kulinda afya za binadamu na mazingira ofisi iliweza kutoa elimu kwa watumiaji wa kemikali zaidi ya 300 kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo kwa wachimbaji wa dhahabu ambao hutumia kemikali nyingi zikiwemo zebaki na cyanide wakati wa kuchenjua dhahabu.

Elimu hii vilevile iliweza kutolewa kwa wajasiliamali wadogo wadogo wanaojihusisha na utengenezaji wa sabuni na batiki ili watumie kemikali kwa usahihi bila kuleta madhara ya kiafya kwa watumiaji na jamii inayowanzunguka.

Ununuzi wa mitambo ya kufanyia uchunguzi wa kimaabara.

Serikali inayoongozwa na Mh. Dkt. Samia S. Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwezesha Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kupata mitambo ya kisasa kwa ajili ya uchunguzi wa sampuli za udongo kubaini kiasi cha dhahabu kwa wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa ili kuongeza tija na ufanisi katika uchunguzi wa sampuli.

Mitambo ambayo imenunuliwa ni Atomic Absorption Spectrophotometer(AAS), X-Rays Fluorescence Spectrometer na DR 6000.

Uchunguzi wa kimaabara wa sampuli/ vielelezo Katika kipindi cha mwezi Machi, 2021 hadi Oktoba 2023, Ofisi ya Kanda ilipokea jumla ya sampuli 547 kwa ajili ya uchunguzi wa wa sampuli mbalimbali za kimaabara kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwemo Jeshi la Polisi, Mawakili, Ustawi wa Jamii na watu binafsi kutoka mkoa wa Mbeya.

Uchunguzi wa sampuli hizi hufanyika katika kutatua changamoto mbalimbali kwenye jamii ikiwemo kubaini waharifu wa ubakaji, wizi na ujambazi na kubaini aina ya dawa za kulevya kwa mshukiwa aliyekamatwa na vitu vidhaniwavyo kuwa ni dawa za kulevya.

Matokeo ya uchunguzi huo yalisaidia Serikali na Mamlaka nyingine za usimamizi/udhibiti kufanya maamuzi baada ya uchunguzi huo kukamilika.


Washiriki wa mafunzo ya matumizi salama ya Kemikali wakimsikiliza mwezeshaji wa mafunzo Georgina Kilindo (kulia) akitoa mada kuhusu matakwa ya Kanuni za Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani za mwaka 2020 kwa wachimbaji wa dhahabu na wauzaji wa kemikali wilayani Chunya.


Shati lenye matone ya damu kwa ajili ya uchunguzi wa vinasaba (DNA)




# HALMASHAURI YA RUNGWE:

## Tumetekeleza kikamilifu miradi ya maendeleo



JAFFAR HANIU - MKUU WA WILAYA YA RUNGWE



ALLY SAID KIUMWA - KATIBU TAWALA RUNGWE

**Na KOKU DAVID-**
*RUNGWE*

WILAYA ya Rungwe kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa Maendeleo inatekeleza malengo na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa kuzingatia, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 – 2025.

Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Mhe.Dkt Samia Suluhu Hassan imefanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Miradi ya Elimu, Afya, Kilimo, na Ufugaji imekamilishwa katika maeneo mbalimbali huku serikali ikianzisha mingine ili kuwasogezea huduma wananchi katika maeneo yao wanayoishi na hivyo kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mpainduzi (CCM).

### SEKTA YA ELIMU.

Kupitia Mpango wa BOOST, Serikali imetoa kiasi cha Tshs. million 970.5 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia katika shule mbalimbali za msingi. Shule zilizonufaika na Mpango huu ni pamoja na shule ya msingi Masebe, Bulyaga, Katumba II, Goye, Mwankeja, Ikuti, Ibililo pamoja na Ujenzi wa Shule mpya ya Kibumbe iliyopo katika kata ya Kiwira.

Shule mpya ya Kibumbe ina jumla ya vyumba 16 vya madarasa, Jengo la utawala, Madarasa ya awali, vyoo na maeneo ya michezo kwa ajili ya kuwajengea uchangamshi wanafunzi wa elimu ya awali. Ujenzi wake umegharimu kiasi cha Tshs. million 538.5 mpaka kukamilika kwake.

Shule hii imeondoa kadhia ya wanafunzi kurundikana katika chumba kimoja kwa shule zilizopo katika kata hii ikiwa ni pamoja na kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu pamoja na kupunguza ajali mbalimbali zilizokuwa zikitokea kutokana na kuvuka barabara kuu iendayo nchi jirani ya Malawi.

Kupitia mpango wa SEQUIP Serikali imejenga shule mpya ya sekondari ya Msasani One kwa gharama ya zaidi ya Tshs. million 470 na mradi umekamilika na kuanza kutoa huduma ya elimu kwa wanafunzi wa kata ya Msasani na maeneo ya jirani. Shule ina vyumba vya madarasa, maabara, jengo la TEHAMA, Utawala, maktaba na vyoo.

### SHULE MPYA YA SEKONDARI LUPEPO

Shule kama hii inaendelea na ujenzi katika kata ya Lupepo kwa gharama ya Tshs. million 538.5 na ujenzi wake upo katika hatua ya ukamilishaji.

Haya ni mafanikio makubwa kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa wakazi wa Wilaya ya Rungwe ambapo miradi mingi ya elimu imetekelezeka kwa weledi na ufanisi mkubwa na matokeo yameanza kuonekana.

Baada ya ukarabati wa shule kongwe ya Sekondari ya Rungwe kukamilika kwa gharama ya Tshs. million 700 ufaulu kwa wanafunzi umeongezeka kwa kiwango kikubwa na kwamba katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kumaliza kidato cha sita kwa miaka miwili mfululizo ya 2022/2023 shule hiyo hakuna wanafunzi waliopata matokeo ya daraja la nne wala sifuri na hivyo kubakiwa na daraja la Kwanza, Pili na



MPOKIGWA MWANKUGA-MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



RENATUS MCHAU - MKURUGENZI HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE






KIBUMBE SHULE MPYA KUPITIA MPANGO WA BOOST



**Mlima Rungwe uliopo wilayani Rungwe ndiyo Mlima Mrefu kuliko yote katika mikoa ya Nyanda za juu kusini na wa tatu nchini Tanzania baada ya Kilimanjaro na Meru (2981m kutoka usawa wa bahari.**



SHULE MPYA YA MSASANI ONE

# HALMASHAURI YA RUNGWE: Tumetekeleza kikamilifu miradi ya maendeleo

Tatu tu.

Mpango wa shule ni kufuta daraja la tatu na kubakiwa na madaraja mawili ya juu katika ufaulu.

**SEKTA AFYA**

Katika sekta ya Afya Serikali imefanikiwa kujenga vituo vitatu vya afya ili kuwasogezea wananchi huduma za matibabu karibu na makazi yao. Vituo hivyo ni kituo cha afya Kyimo, na Ndanto ambavyo vimekamilika na tayari vinatoa huduma kwa wagonjwa huku kituo cha afya cha Iponjola kikiwa katika hatua za ukamilishaji. Vituo vyote hivi kila kimoja kimegharimu zaidi ya Tshs. million 500 lakini pia vituo hivyo tayari kila kimoja kimepokea Tshs. million 25 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Aidha katika robo hii ya kwanza mwaka wa fedha 2023/24 serikali imetoa kiasi cha Tshs. bil. 1 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vipya vya afya katika kata za Kiwira na Masoko.

Wakati huohuo kupitia mradi wa GLOBAL FUND Serikali imetoa kiasi cha Tshs. million 271 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na nyumba ya mtumishi katika zahanati ya Masoko iliyopo kando ya Ziwa Kisiba.

**UPANUZI WA ZAHANATI VIJIJINI**

Serikali hii Tukufu haijawaacha kando wakazi wa Kakindu, Lufumbi, Simike, Swaya, Nkunga na Ilenge kwani zahanati zao zimekamilika na zinatoa huduma stahiki kwa afya na maendeleo ya wananchi. Kila zahanati ilipata kiasi cha Tshs. million 50 kwa ajili ya ukamilishaji. Zahanati ya Matwebe na Kyosa zipo katika hatua ya ukamilishaji.

Mama Samia Suluhu Hassan Rais wa Watanzania wote ametoa kiasi cha Tshs. bil. 1 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) katika hospitali ya Wilaya ya Tukuyu. Jengo hili linatarajiwa kuwa na ghorofa zaidi ya moja na litajumuisha pia ofisi na wodi za kulaza wagonjwa.





Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa Dharula (EMD) katika hospitali hii pia umekamilika kwa gharama ya Tshs. million 326 hatua iliyotatua changamoto ya wagonjwa wanaotokana na athari za moto, ajari, magonjwa ya mlipuko kama COVID kutibiwa haraka na kuendelea na shughuli za ujenzi wa taifa wakiwa na afya bora.

Halmashauri ya Rungwe kwa kutumia mapato yake ya ndani katika msimu wa robo ya kwanza imetoa kiasi cha Tshs. million 535,382,729.07 kwa ajili ya utekelejaji wa miradi mbalimbali.

Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa stendi ya daladala katika mji wa Tukuyu, ununuzi wa gari la kuzolea taka, ukamilishaji wa zahati ya Lufumbi na kituo cha afya cha Kyimo, ukamilishaji wa miundombinu ya sekondari Msasani One, ujenzi wa shule mpya ya mchepuo wa kingereza katika eneo la Ilenge, ukarabati wa nyumba za watumishi na ofisi ya kata ya Kisondela, ununuzi wa pikipiki nne na machine za kukusanyia mapato (POS).

**SEKTA YA KILIMO**

Kutokana na uzuri wa hali ya hewa katika halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Sekta ya Kilimo inachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Wilaya na kwamba zaidi ya asilimia 90 ya pato la Wilaya linatokana na kilimo.

**ENEO LINALOFAA KWA KILIMO NI HEKTA 92,389.5**

Mazao makubwa ya biashara ni kahawa, chai na kokoa huku mazao ya chakula yakiwa ni ndizi, mahindi, viazi mviringo, viazi vitamu, maharage na mpunga.

Wakulima wanaopata huduma za ughani wameongezeka kutoka wakulima 66,387 mwaka 2020 na kufikia 70,105 Aprili, 2023.

Uwiano wa wakulima wanaotumia mbolea za viwandani umeongezeka kutoka 76% mwaka 2020 hadi kufikia 81% mwaka 2022.

Viwanda vitatu vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo vimejengwa na kwamba hadi kufikia 2023 wastani wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara umeongezeka kama ifuatavyo:-

Mahindi yalikuwa yakizalishwa tani 102,945 mwaka 2020 lakini yameongezeka na kufikia tani 103,990 Juni, 2022.

Kwa upande wa ndizi zilikuwa zikizalishwa tani 352,848 mwaka 2020 lakini yameongezeka hadi kufikia tani 356,404.0 mwaka 2022.



KITUO CHA AFYA KYIMO



Ujenzi wa Standi mpya ya Standi ya Daladala Tukuyu

Katika sekta ya Afya Serikali imefanikiwa kujenga vituo vitatu vya afya ili kuwasogezea wananchi matibabu karibu na makazi yao. Kituo cha afya Kyimo, na Ndanto vimekamilika na tayari vinatoa huduma...



## BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)
### OFISI YA NEMC NYANDA ZA JUU KUSINI MKOA WA MBEYA

# NEMC MBEYA: Ndani ya miaka miwili ya awamu ya sita tumesajili zaidi ya miradi 100 ya uwekezaji





Meneja wa Kanda na maafisa wakitoa elimu kupitia Redio (Highland FM) na katika soko la Uyole.

**Na KOKU DAVID-**
*MBEYA.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia ofisi yake ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mkoa wa Mbeya inatekeleza shughuli mbalimbali za uhifadhi na kusimamia mazingira kulingana na sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Kwa kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hasan, Baraza limehakikisha kuwa Mazingira yanalindwa, yanatunzwa lakini pia kutoa elimu kwa wananchi kutambua jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi kulinanga na Sura ya Pili ya Kifungu cha 18 (b) (vii) cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi kinavyoelekeza.

Ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi hasa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya Nchi, ofisi ya Kanda imefanya kaguzi mbalimbali katika Migodi, Viwanda na maeneo ya biashara ili kuhakikisha miradi yote ya uwekezaji inafanya shughuli zake bila kuathiri mazingira.

Kanda pia imekuwa ikitoa elimu na kuwaelekeza wawekezaji kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira au Kaguzi za Athari kwa Mazingira ili kupata vyeti vya Mazingira.

Katika kipindi cha miaka miwili, Baraza limeendelea kusajili na kutoa vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa Miradi ya Uwekezaji iliyopo katika Mkoa wa Mbeya, Kutoa elimu ya utunzaji na kusimamia mazingira kupitia vyombo vya habari, mikutano ya hadhara na katika matukio ya Kimataifa kama vile nanenane na siku ya Mazingira Duniani.

Baraza pia limetekeleza na kusimamia maelekezo yanayotolewa na viongozi mbalimbali wa Serikali katika Mkoa wa Mbeya. Baraza pia katika Mkoa wa Mbeya limefanikiwa kushughulikia malalamiko kutoka kwa wadau na wananchi ambayo yamekuwa yakiwasilishwa ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Ili kuboresha mazingira ya uwekezaji, Baraza lina mfumo wa kielektroniki wa kusajili miradi (PMS) ambao unasaidia wawekezaji kusajili miradi na kupata cheti cha Tathmini za Athari kwa Mazingira kwa uharaka zaidi. Kwa kipindi cha miaka miwili, Baraza limefanikisha kusajili zaidi ya miradi 100 ya uwekezaji, ndani ya mkoa wa Mbeya na kufanikiwa kupata vyeti vya TAM.

Kupitia TAM wawekezaji wameweza kusimamia na kutunza mazingira katika maeneo yao ya kazi, hivyo kupunguza migogoro na uchafuzi wa mazingira.

Baraza limetoa elimu ya vibali vinavyotolewa kwa ajili ya kukusanya, kusafirisha na kutunza taka hatarishi (Vyuma chakavu, Mafuta machafu, taka za kielektroniki na makopo yanayobeba kemikali).

Elimu imekuwa ikitolewa kwa kuwakutanisha wadau wanaojishughulisha na shughuli za taka hatarishi lakini pia kukagua maeneo yao ya biashara ili kuona ni namna gani wanafuata taratibu za Serikali zilizowekwa.

Usimamizi na utoaji wa vibali vya taka hatarishi unasaidia kutoharibiwa kwa miundombinu ya nchi kama vile barabara, reli, mifumo ya umeme na maji hali kadhalika kuondoa na kupunguza uchafuzi wa Mazingira.

Baraza limendelea kutoa elimu ya katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki kulingana na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki na Lakiri za vifuniko vya Plastiki za Mwaka 2022.

Elimu hii imetolewa katika vyombo vya Habari na kuwafikia wananchi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya yakiwemo na maeneo ya masokoni kama vile Uyole, Soweto, Kabwe na Mbalizi.

Ili kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha na kusimamia ubora wa Maji, Baraza kwa kushirikia na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, na Shirika la Misitu Tanzania (TFS) limepanda miti takriban 1500 ambayo ni rafiki kwa mazingira katika vyanzo vya maji vya maeneo ya Ituha na Kawetele.

Baraza linatekeleza haya ili kuhakikisha vyanzo vya maji haviendelei kuathirika na kusababisha kupungua kwa uwingi na ubora wa maji.

Baraza lina jukumu la kulinda na kutunza Mazingira kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla. Hivyo, uharibifu wa mazingira hasa vyanzo vya maji kunasababisha athari mbalimbali ikiwemo Mafuriko, kuharibu uoto wa asili na ikolojia ya wanyama na mimea.

Baraza limekuwa likitoa elimu ya Mazingira kwa wadau mbalimbali zikiwemo Klabu za Mazingira za wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari na Vyuo.

Siku ya Mazingira Duniani, 5/Juni/2023, Baraza kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Kyela walizindua Klabu ya Mazingira iliyoanzishwa katika shule ya msingi Sama iliyopo Wilaya ya Kyela.

Klabu za mazingira mashuleni na vyuoni kwa kushirikiana na walimu wao zimekuwa zikisaidia katika kutunza Mazingira na kutoa elimu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi katika maeneo yao.

Baraza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Mazingira liliandaa zoezi la kufanya usafi ili kuhamasisha jamii iweke kipaumbele cha kusafisha maeneo yao kwa mujibu wa taratibu mbalimbali za kimazingira.

Baraza katika wiki ya siku ya Mazingira Duniani Juni 2022 lilifanya usafi katika maeneo ya stendi kuu Mbeya, Soko la Soweto na Wilaya ya Mbarali katika eneo la Igawa pembezoni mwa barabara.

Katika wiki hiyo pia elimu ilitolewa kwa watumiaji wa usafiri wa barabarani kutoka Mbeya hadi Njombe na Iringa kutotupa taka hovyo barabarani pindi wawapo safarini.

Baraza limekuwa likishughulikia na kutoa elimu kuhusiana na katazo la mitetemo na sauti zilizozidi viwango katika Mkoa wa Mbeya ili kuhakikisha mitetemo na sauti zinazotolewa haziathiri afya ya binadamu na kusababisha kero kwa wakazi na wananchi.

Katika swala hili Baraza limeweza kufanya vikao na wadau mbalimbali kwa kutoa elimu ya viwango vya kelele vinavyokubalika katika maeneo ya makazi, biashara na viwandani.

Elimu ya mazingira imeendelea kutolewa kwa wadau kupitia vikao vya mabaraza ya biashara ya Mkoa.

Kwa kipindi cha miaka miwili jumla ya malalamiko 40 yamepokelewa na kushughulikiwa.

Malalamiko hayo yalihusiana sana na;
Utililishaji ovyo wa maji taka
Kelele (Sauti zilizozidi viwango)
Uharibifu wa vyanzo vya maji
Utupaji ovyo wa taka

Baraza limeshiriki katika maonyesho ya Kimataifa ya Kilimo (nanenane 2022 na 2023) yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya ili kutoa elimu ya utunzaji na uhifadhi wa Mazingira kwa wadau na wananchi mbalimbali wakiwemo wakulima ili kuwa na kilimo endelevu kinachozingatia utunzaji na uhifadhi wa Mazingira.

Katika Banda la NEMC, viongozi, wadau mbalimbali, wananchi hata vikundi vya wanafunzi waliweza kutembelea na kujifunza kazi za Baraza na jinsi ya kutunza Mazingira.

Pia elimu ya usajili wa miradi kwa njia ya mtandao ilitolewa kwa wadau na wawekezaji waliotembelea banda la NEMC.

Baraza pia limekuwa linasimamia mifumo ya Ikolojia kwa kuhakikisha shughuli za kibinadamu haziathiri Milima, Misitu, Mito na Maziwa.

Kwa kutekeleza hili Baraza liliweza kutembelea baadhi ya maeneo kavile Mlima wa Living Stone iliyopo katika Wilaya ya Rugwe ili kuelimisha jamii inayoishi pembezoni kwa mlima huo kutoathiri uoto wa asili wa mlima huo.

Baraza pia limekuwa likifanya kaguzi mbalimbali za Mazingira katika miradi ya maendeleo Mkoa wa Mbeya na kutoa elimu ya uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake.






Waziri Mkuu Mstafu akiwa katika Banda la NEMC na wadau mbalimbali ili kupata elimu ya Mazingira.



Inaonyesha Kaimu Mkuu wa wilaya akimwagilia mti wa mfano alioupanda na pia kikundi cha wanafunzi ambao ndiyo Klabu ya Mazingira.

## MAFANIKIO YA MKOA WA MBEYA KATIKA SEKTA YA MADINI

# ACHIMWENE: Serikali Awamu ya Sita imerahisisha biashara ya madini



Mkuu wa mkoa wa Mbeya Juma Homera alipotembelea Mgodi wa Kampuni ya Achimwene Busness Group Co. Ltd



Mtambo wa Mgodini

**Na KOKU DAVID** - *Chunya*

Kampuni ya Achimwene Busness Group Co. Ltd ni kampuni inayojishughulisha na uchimbaji mdogo mdogo wa madini mkoani Mbeya katika Wilaya Chunya.

Kampuni hiyo imekuwa mkombozi kwa vijana kwani imekuwa ikitoa ajira kwa vijana kutoka katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na Uhuru ya Kijani, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Achimwene Busness Group Co. Ltd Henerico Yohana anasema kuwa kupitia Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kampuni yake inayojishughulisha na uchimbaji mdogo mdogo wa madini imeweza kurahisisha masoko ya biashara ya madini hali inayosababisha vijana wengi kupata ajira na kipato kuendesha maisha yao.

Anasema, soko la pamoja la kuuzia madini limesaidia kupaisha bei ya dhahabu na kupata faida baada ya mtu kuuza dhahabu zake.

Anasema kutokana na hali hiyo, imemuwezesha kutoa ajira kwa vijana wenzake ikiwa ni pamoja na kusaidia jamii inayozunguka eneo analochimbia dhahabu.

Anaongeza kuwa, jambo kubwa kuliko yote wanaishukuru serikali kupeleka umeme katika Kijiji cha Itumbi ambako wanafanyia uchimbaji hali iliyosaidia kuendesha mitambo yao kwa faida.

Anasema kabla ya kuwekewa umeme kwa mwezi walikuwa wakitumia Tshs. milioni 30 hadi Tshs. milioni 45 kununua dizel lakini hivi sasa wanatumia Tshs. milioni 8 mpaka Tshs. milioni 9.

Anasema jitihada za serikali katika kuwatengenezea mazingira mazuri ya biashara imewaondoa kwenye kutumia Tshs. milioni 45 kwa ajili ya mafuta kila mwezi hadi kutumia gharama za chini ya kiwango cha kawaida kabisa.

"Napenda kuishukuru sana serikali ya yetu ya Awamu ya Sita chini ya mama yetu Samia Suluhu Hassani kwa kutukumbuka na kutupa kipau mbele sisi wafanyabiashara wa madini kwani pamoja na kutuletea umeme lakini soko la madini na kufungua milango ya kuuza madini limesaidia bei ya dhahabu kupanda na kutupatia faida," anasema Heneriko.

Anasema, kabla ya kuwepo kwa soko la madini biashara ilikuwa ni ya ubabaishaji na kwamba watu walikuwa wakinunulia mitaani dhahabu hali iliyokuwa ikichangi kuzulumiwa tofauti na sasa baada ya kuanzishwa kwa masoko ya madini.

Anasema changamoto nyingine walizokuwa wakikutana nazo ni kutoaminika katika mabenki na kushindwa kukopesheka sababu kubwa ikiwa ni kukosekana kwa soko la uhakika la kuuza dhahabu.

"Kwakweli kukosekana kwa soko la uhakika la dhahabu kulichangia sana sisi kutoaminika na kuonekana kama wahuni.

"Hapakuwan a sehemu ya kuzipeleka dhahabu na badala yake zilikuwa zinauzwa pembeni au uchocholoni lakini sasa hivi tunaishukuru serikali kwa kutuletea soko la uhakika hali ambayo imesaidia kuanza kuaminika na kukopesheka," anasema Heneriko.

Tangu lipatikane soko la madini, anasema biashara imekuwa ya uwazi kila mtu anaona na imesaidia unafuu wa kukopesheka lakini pia bei imekuwa nzuri hivyo wafanyabiashara wa madini hawana shida tena na masoko.

Heneriko anasema hivi sasa biashara hiyo ya madini imekuwa tegemezi kwa jamii kutokana na faida inayopatikana baada ya mauzo kupitia soko la madini.

Anaongeza kuwa, kutokana na biashara ya madini vijana wengi wameweza kufanya shughuli nyingine mbalimbali za kuwaingizia kipato.

Anasema kupitia biashara hiyo ya madini, ameweza kufungua kampuni ya usafilishaji ikiwa ni pamoja na kuisaidia jamii katika mambo mbalimbali ya maendeleo.

Kupitia uchimbaji mdogo mdogo anaoufanya, anasema pamoja na kutoa ajira kupitia kampuni yake pia amesaidia sehemu ya ujenzi katika shule ya msingi Itumbi na sekondari ambayo hivi sasa ipo katika hatua za awali za ujenzi pamoja na ujenzi wa Zahanati katika Kijiji hicho.

Anasema, pia kampuni yake mara kwa mara imekuwa ikitoa huduma za maji katika vituo vya Afya vilivyopo jirani na Kijiji ambacho mgodi wake upo.

"Hatujafanya mambo mengi kwa jamii lakini haya machache tunayofanya ni kwa sababu tu ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita ambayo imetuwekea mazingira mazuri ya biashara lakini pia na uongozi wa Mkoa wa Mbeya wanaotupa ushirikiano mzuri pamoja na mkuu wa Wilaya ambao kwa pamoja wapo karibu sana na sisi wafanyabiashara wa madini," anasema Heneriko.


Anasema kuwa katika kurudisha shukrani kwa serikali, kampuni yake pia hushirikiana vizuri na uongozi wa Kijiji ili kuhakikisha maendeleo yanapatikana katika eneo hilo.

Anasema kiujumla anaipongeza serikali kwa namna ilivyo karibu na wawekezaji lakini pia imewaondolea hofu kwani hivi sasa wana uwezo wa kuzungumza na watendaji wakuu wa serikali mambo mbalimbali kulingana na biashara zao.

"Kwa mara nyigine nampongeza sana mama yetu Dkt. Samia kwa kutoa kipaumbele kwa sisi wachimbaji lakini pia amechangia kwa kiwango kikubwa maendeleo ya Chunya," anasema Heneriko.



Mtambo wa Mgodini




# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo


MAYEKA S.MAYEKA - MKUU WA WILAYA YA CHUNYA


ANAKLETH MICHOMBERO- KATIBU TAWALA CHUNYA

**Na KOKU DAVID-**
*CHUNYA.*

Halmashauriya Wilaya ya Chunya ni Halmashauri iliyo ndani ya wilaya ya Chunya ambayo ni kati ya Wilaya tano zilizopo mkoani Mbeya. Wilaya ya Chunya inapakana na Mkoa wa Singida na Tabora kwa upande wa Kaskazini, Mkoa wa Iringa na wilaya ya Mbarali kwa upande wa Mashariki, Wilaya ya Songwe kwa upande wa Magharibi.

Wilaya ya Chunya iko umbali mita 800 mpaka mita 1500 kutoka usawa wa Bahari na iña joto kati ya nyuzi joto 21C mpaka 23 C. Wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya milimita 700 na 1200 kwa mwaka.


KITUO CHA AFYA SANGAMBI

Wilaya ya Chunya ilianzishwa miaka 1930 na baadaye mwaka 1984 ndipo Halmashauri ya wilaya ya Chunya ikaanzishwa rasmi wakati serikali za mitaa zilipoundwa. Makao makuu ya wilaya ya Chunya yako Chunya Mjini ambapo kata za Itewe na Chokaa ndizo kata zinazounda makao makuu ya wilaya hiyo.

**ENEO LA ARDHI**

Wilaya ya Chunya ina ukubwa wa eneo wenye jumla ya kilometa 13,149 ambapo Tarafa ya Kipembawe ina ukubwa kilometa 8,766 sawa na asilimia 66.9 za eneo la wilaya wakati Tarafa ya kiwanja ina kilometa 4,383 sawa na asilimia 33.3. Katika kata 20 zinazounda wilaya ya Chunya kata ya Mafyeko ndio kata yenye eneo kubwa kuliko zote na kwamba inachukua asilimia 25.9 za eneo la Wilaya ikifuatiwa na Kambikatoto ambayo ina asilimia 15.9 huku kata ya Itwete ikiwa na asilimia 0.5 ya eneo lote la Wilaya ya Chunya.

Asilimia 87 ya wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya wanategemea kilimo na Kilimo ndiyo huchangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wa wilaya na kwamba yapo mazo mbalimbali ya biashara ambayo hulimwa katika Wilaya hii ya Chunya ambayo ni Tumbaku, Alizeti, karanga, soya na mengine lakini mazao kuu la biashara ni Tumbaku ambalo kwa Mwaka 2021/2022 tani 7,000 za Tumbaku zilizalishwa wakati mwaka 2022/2023 tani 18,000 za Tumbaku zimezalishwa.


UWANJA WA MPIRA WA MIGUU CHUNYA


SHULE YA ENGLISH MEDIUM.

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pia inayo skimu ya umwagiliaji Ifumbo ambayo ina hekta 600 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kwamba mazao kama Mpunga, maharage, Mboga mboga na mazao mengine hulimwa.

Mpaka sasa eneo linalotumika kwa kilimo ni hekta 141 na kwamba gharama zilizotumika kujenga skimu hiyo ya umwagiliaji ni Tshs. milioni 915,000,000 kutoka kwa wadau mbalimbali ambao ni ASDP/DADP's, DIDF/NIDF pamoja na Halmashauri ya Wilaya.

**UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI**

Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 makisio kwa mwaka yalikuwa ni kukusanya Tshs. bil. 4,846,560.000.00 lakini zilikusanywa Tshs. bil. 5,271,993,916.70 ambazo ni sawa na asilimia 108.78.

Mwaka 2022/2023 makisio yalikuwa ni kukusanya Tshs. bil. 5,330,600,000.00 lakini zilikusanywa Tshs. bil. 6,279,902,160.35 ambazo ni sawa na asilimia 117.81. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Makisio ya makusanyo ni Tshs. bil. 5,543,358,000.00 mpaka kufikia Octoba 2023 Halmashauri ya wilaya Imekusanya Tshs. bil. 2,967,876,117.64 ambayo ni sawa na asilimia 53.54

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI**

Sekta ya Michezo na Burudani.

Halmashauri ya wilaya ya Chunya inajenga uwanja wa Halmashauri ambao ndani yake utakuwa na viwanja mbalimbali kama vile uwanja wa mpira wa miguu, Uwanja wa Mpira wa pete, Uwanja wa mpira wa Mikono (Handball), na viwanja vingine vingi. Uwanaja huo unatarajiwa kughalimu kiasi cha Tshs. bil. 10,031,933,405.00.

Hadi sasa ujenzi wa uwanja huo umeshaghalimu kiasi cha Tshs. bil. 1,883,851,252.84 ambapo chanzo cha fedha kilichotumika ni mapato ya ndani pamoja na michango ya wadau wa maendeleo.

Uwanja huo unaosimamiwa na kumilikiwa na Halmashauri, mpaka sasa shughuli zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa ukuta ambao umeghalimu Tshs. milioni 34,160,800 na kwamba kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri imetenga Tshs. milioni 70 ambapo kati ya fedha hizo mpaka sasa Tshs. milioni 34,726,500 zimeshatumika. Aidha, shughulizi zinazoendelea kufanyika kwa sasa katika pesa hizo zilizotengwa mwaka 2023/2024 ni kujenga nguzo 91 pamoja na maandalizi ya eneo la kuchezea kwa viwanja vyote.

**SEKTA YA AFYA.**

Kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 Halmashauri ilipokea Jumla ya Tshs. bil. 4,203,000,000.00 kwaajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali na kwamba katika fedha hizo Tshs.bil. 2,890,000,000.00 zilipokelewa toka Serikali Kuu, Tshs. mil. 500,000,000.00 fedha za TOZO za Miamala za simu, Tshs. mil. 490,000,000.00 mapato ya ndani, fedha za UVICO Tshs. mil. 300,000,000.00 na Tshs. milioni 23,000,000 Global fund


BOSCO MWANGINDE - MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA


TAMIM H.KAMBONA - MKURUGENZI HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

**SEKTA YA ELIMU.**
**ELIMU SEKONDARI**

Kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. bil. 3,057,452,407.85 zikiwa ni fedha kutoka Serikali Kuu, SEQUIP, EP4R, UVIKO 19, TOZO na Pochi la Mama kwaajili ya utekelezaji na Ukamilishaji wa miundombinu mbalimbali ya elimu.

**ELIMU MSINGI NA AWALI**

Kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. bil. 4,585,735,760.00 kutoka Serikali Kuu, EP4R, UVIKO19, LANES II na BOOST kwaajili ya Ukamilishaji na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu Msingi na Awali.

Uwezeshaji wananchi Kiuchumi.

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imekuwa ikiwawezesha wananchi kiuchumi kupitia utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na kwamba kuanzia mwaka wa fedha wa 2020/2021 hadi 2022/2023 kiasi cha Tshs. bil. 1,009,195,000.00 kilitolewa kama mkopo kupitia mapato ya ndani.

Pia katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 hadi 2022/2023 kiasi cha Tshs. bil. 1,686,852,594.00 kilitolewa kama mkopo wa jumla kupitia mapato ya ndani na mapato kutoka serikali kuu.

# TALIRI UYOLE:

## Tunajivunia kuboresha uzalishaji endelevu wa mifugo



**Ng'ombe aina ya Friesian wanaopatikana kituoni TALIRI Uyole**

**Na Koku David** - *Mbeya.*

Taasisi Ya Utafiti Wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Uyole ni miongoni mwa vituo nane (8) vya Kanda vinavyounda TALIRI ambayo ilianzishwa chini ya Sheria No. 4 ya 2012. TALIRI Uyole inasimamia shughuli za utafiti katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini) na kwamba ipo takribani kilometa 11 kutoka mji wa Mbeya, pembezoni mwa barabara kuu ya Tanzania/ Zambia (TANZAM).

Taasisi hii inasimamia kikamilifu utafiti wa mifugo nchini ili kuongeza uzalishaji na kipato kwa wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla wake.

Dira ya TALIRI ni kuwa Taasisi ya Mifugo ya mfano inayochangia kuboresha hali ya maisha ya wafugaji na wadau wengine na Dhima yake ni kutengeneza, kusambaza na kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi kwa wadau wote wa mifugo ili kuboresha uzalishaji endelevu wa mifugo.

**MAJUKUMU MAKUU YA TAASISI NI KAMA IFUATAVYO:**

Kutunza na kusambaza aina bora za ng'ombe wa maziwa waliopo Kituoni kwa wafugaji wadogo katika Kanda.

Kuibua tekinolojia bora na muafaka za ufugaji kwa aina mbalimbali za mifugo ikiwa pamoja na ng'ombe, nguruwe, kuku na wanyama wengine wadogo watakaoonekana wana umuhimu katika Kanda na Taifa kwa ujumla. Teknolojia hizi zinahusu mifumo ya menejimenti ya mifugo, usindikaji na matumizi ya mazao ya mifugo yenye kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Kutafiti na kukuza matumizi ya malisho ya mifugo ili kuboresha lishe na uzalishaji wa mazao ya mifugo.

Kuendeleza na kuhifadhi mifugo ya asili kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa nyama na mazao mengine ya mifugo.

Kuimarisha mahusiano kati ya watafiti, maafisa ughani, wafugaji na wadau wengine katika Kanda ili matokeo ya tafiti za mifugo ziwafikie walengwa.



**Kuku aina ya Kuroiler**

**MAFANIKIO.**

Kituo cha Utafiti wa Mifugo cha Uyole kimepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa malengo ya utafiti katika Kanda. Baadhi ya mafanikio hayo ni yafuatayo:

Kituo kimefanikiwa kusambaza mbegu za ng'ombe kwa kusambaza madume na majike kwa wafugaji wadogowadogo na Asasi za serikali na zisizo za kiserikali. Usambazaji wa mbegu za ng'ombe bora wa maziwa kumeleta muamko mkubwa katika Kanda kwa kufuga aina hii ya ng'ombe ili kuongeza kipato na kuboresha lishe za familia. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi sasa ng'ombe bora 57 (majike 8 na madume 49) walisambazwa kwa wafugaji wa mikoa ya Mbeya, Njombe, Dar-Es-Salaam, Songwe, Iringa na Ruvuma.

Uzalishaji wa mbegu za malisho aina ya Rhodes (Chloris Gayana) pamoja na mikate ya majani (Hay bales). Kiasi cha Tani 2.5 za mbegu kilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wa mikoa mbalimbali nchini. Na kiasi cha marobota (Bales) 10,000 kilizalishwa na kuuzwa kwa wafugaji wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kiasi kingine kililishwa kwa mifugo iliyopo kituoni. Pia kituo kina majani aina mbalimbali za Mabingobingo (Napier) ambayo yanazalishwa na kulishwa kwa mifugo. Pia vipando vya mbegu hizi husambazwa kwa wafugaji walio na mashamba kwa ajili ya kupanda.



**MPANGO MKAKATI.**

Tafiti mbalimbali za kuku wa asili na chotara, ambapo kuku aina ya Mandendenga na Katewa walifanyiwa tafiti. Kwa sasa kuna kuku wa asili aina ya Horasi na kuku chotara aina ya Kuroiler ambao wanafanyiwa utafiti na kutunzwa. Utafiti wa nguruwe pia unafanyika kituoni kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza kwa wafugaji. Nguruwe aina ya Large White, Duroc na chotara wake wanafugwa kwa lengo la kufanya tafiti na kuzalisha.

Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Uyole pia inatoa mafunzo kwa vitendo kwa wafugaji na wanafunzi wa mifugo kutoka vyuo vya mifugo. Kwa mwaka 2023 taasisi ilipokea jumla ya wanafunzi 60 kutoka vyuo vya LITA Morogoro, LITA Madaba na SUA kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa muda wa miezi miwili. Pia taasisi imekuwa ikipokea wafugaji mmoja mmoja na makundi ya wafugaji kwa ajili ya kutoa elimu mbalimbali za ufugaji.



**Mikate ya majani (Hei)**



**Wanafunzi wakielekezwa namna ya kupanda malisho aina ya mabingobingo (Napier)**



**Mikate ya majani (Hei) ikitolewa shambani na kupelekwa kuhifadhiwa kwa ajili ya kulishia mifugo na kuuzwa kwa wafugaji wakati wa kiangazi.**



**Ng'ombe aina ya Friesian wanaopatikana kituo cha TALIRI Uyole**

## MAFANIKIO YA MKOA WA MBEYA KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

# TIRA MBEYA:

## SEKTA YA BIMA YAZIDI KUIMARIKA




Baadhi ya wananchi waliohudhuria katika maonesho ya Nanenane 2023 Jijini Mbeya wakipatiwa elimu ya bima katika banda la TIRA.

**Na KOKU DAVID-** *Mbeya*

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inatekeleza Majukumu yake kupitia Ofisi na Kanda zake mbalimbali ikiwemo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ina ofisi yake mkoani Mbeya. Yafuatayo ni mafanikio ya Sekta ya Bima chini ya uongozi wa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.



Wakulima Kata ya Kajunjumele wilayani Kyela wakipatiwa elimu ya bima ya kilimo.




Wanafunzi wakipatiwa elimu ya bima wakati wa maonesho ya nanenane 2023 Jijini Mbeya.

**UELIMISHAJI WA BIMA KWA WATANZANIA:**

Chini ya uongozi wa Serikali ya awamu ya Sita, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima imeweza kuwafikia wananchi wengi zaidi katika kutoa elimu ya bima ili kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa masuala yanayohusu bima pamoja na haki zao ambapo zaidi ya wakazi wa jiji la Mbeya 600,764 walipatiwa elimu ya bima katika nyanja mbalimbali kulingana na mahitaji yao.

**UWEKEZAJI WA KUVUTIA:**

Serikali ya awamu ya sita imeweka Mikakati mbalimbali ili kuvutia wawekezaji, kuimarisha mazingira ya biashara, na kutoa motisha ambapo imesaidia kufungua milango ya fursa mpya za uwekezaji katika sekta ya bima.

Kupitia mikakati iliyowekwa na serikali ya awamu ya sita katika kukuza uwekezaji katika sekta ya bima Tanzania, Mamlaka imefanikiwa kuongeza mawakala wa bima wapatao 12 na kupelekea idadi ya mawakala wa bima 33 ndani ya mkoa wa Mbeya kufikia Oktoba, 2023.

Mamlaka inaendelea kuweka mikakati kulingana na maelekezo ya Serikali ili kuhakikisha kuwa wigo wa usambazaji wa bidhaa za bima unatanuka ili wananchi waweze kupata huduma za bima kwa urahisi zaidi popote walipo.

Pia Serikali imeweka mazingira mazuri ya biashara, maboresho ya Sheria, na hatua za kuhamasisha uwekezaji ambazo ni kichocheo katika kuvutia wawekezaji wa kigeni pamoja na kufuta baadhi ya masharti ya usajili kwa mawakala wa bima kikiwemo kigezo cha mtaji ili kuongeza wigo wa watoa huduma za bima kote nchini.

**MAFANIKIO YA KAMPUNI ZA BIMA:**

Mkoa wa Mbeya una matawi ya kampuni za Bima yapatayo 13. Sekta ya bima kwa ujumla illifanikiwa kukusanya ada za bima zenye thamani ya Tsh. 13.7 bilioni katika bima za kawaida na Tsh. 762 milioni katika bima za Maisha ndani ya mkoa wa Mbeya katika kipindi cha mwaka 2022. Takwimu hizi zinaonesha muamko wa wananchi katika kujilinda na athari za majanga mbalimbali kupitia bima na vilevile mchango wa bima katika kuwanusuru watanzania kuondokana na umasikini na kupelekea mustakabali mzuri wa kifedha.

**MAENDELEO YA TEKNOLOJIA:**

Serikali ya awamu ya sita kupitia TIRA imefanikiwa kuleta mabadiliko ya teknolojia ambayo yamelenga kuimarisha usimamizi na usalama wa soko la bima kwa kuboresha mifumo ya digitali. Mamlaka imeboresha Mfumo wa TIRA-MIS ambao unatumika kuhakiki bima mbalimbali na katika maboresho hayo imeleta mabadiliko kwa kuimarisha uhalali wa bima zinazotolewa na kupunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vya udanganyifu kwenye bima.

Vilevile Serikali imerahisisha mifumo ya usajili wa watoa huduma za bima kwa kuanzisha mfumo wa usajili mtandaoni unaopatikana kupitia tovuti ya Mamlaka yenye anuani ors.tira.go.tz. Kupitia mfumo huu Serikali ya awamu ya sita imerahisha njia ambayo wananchi na wawekezaji wanaweza kufanya usajili wa biashara za bima kwa urahisi zaidi.

Watoa huduma za bima zaidi ya 33 ndani ya mkoa wa Mbeya wametumia mfumo huo kikamilifu katika kupata leseni za bi

ashara ya bima ambao ni sawa na asilimia 78.57 ya wakala wa bima walioomba usajili.

**HITIMISHO:**


Sekta ya Bima nchini Tanzania inaendelea kukua chini ya uongozi wa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa Rais Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mafanikio, ukuaji wa uchumi, na mabadiliko chanya yanaendelea kuiweka Tanzania katika ramani ya kimataifa.


Fursa za kipekee, mazingira bora ya biashara, na mikakati madhubuti inayoendelea kuwekwa, inaonyesha jinsi Tanzania inavyoendelea kuwa kitovu cha uwekezaji wa kimataifa ikiwemo uwekezaji katika sekta ya bima.




Namna ya kuhakiki bima kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.




Taswira ya mfumo wa usajili wa watoa huduma za bima (TIRA-ORS)




# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

## yafanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo



JAFFAR HANIU - MKUU WA WILAYA YA RUNGWE



ALLY SAID KIUMWA - KATIBU TAWALA RUNGWE

**Na Peter Tungu-** BUSOKELO.

Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ni miongoni mwa Halmashauri mpya za Wilaya zilizoanzishwa nchini Tanzania na ikiwa imegawanywa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mwaka 2012 baada ya mlolongo wa mageuzi na hitaji la kutoa huduma bora kwa jamii.

**HISTORIA YA KIJIOGRAFIA**

Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo inapatikana kati ya latitudo 80 30 □ mashariki 90 30□ kusini mwa Ikweta na longitudo 33□ na 34□ mashariki mwa mstari wa Greenwich. Halmashauri hii inapakana na Wilaya ya Kyela kwa upande wa kusini, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa upande wa magharibi, Wilaya ya Makete kwa upande wa mashariki na Wilaya ya Mbeya upande wa kaskazini.



Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo yapo Mji wa Lwangwa ambao upo kilomita 47 kutoka Tukuyu mjini.

**ENEO LA ARDHI**

Halmashauri ina jumla ya eneo la kilomita za mraba 969.14 ambapo asilimia 85 ya eneo hilo linatumika kwa ajili ya kilimo wakati ardhi iliyobaki asilimia 15 zikiwa zimetawaliwa na misitu, milima na maeneo ya makazi

**HALI YA HEWA**

Hali ya hewa ya Halamshauri hii inatokana na urefu wake kutoka usawa wa bahari na imepambwa na milima ambapo kuna mlima Rungwe na Livingstonea mbayo ipo mita 770 hadi 2,265 kutoka usawa wa bahari. Wastani wa mvua ni milimita 900 kwenye maeneo ya tambarare hadi milimita 2,700 kwa maeneo yenye miinuko. Kwa kawaida joto linakadiliwa kuwa nyuzi joto 18-25 kwa kipindi chote cha mwaka.

**KANDA ZA KILIMO:**

Halmashauri ya Busokelo imegawanyika katika kanda kuu tatu za kilimo, ukanda wa Chini, Kati na Juu. Katika kanda hizo tatu zinatofuatiana kwa tabia ya hali ya hewa na mazao yanayolimwa kama ifuatavyo;

Ukanda wa chini:

Unaundwa na Kata za Kisegese, Kambasegela, Ntaba, Itete, Lufilyo na sehemu ya kata ya Lupata katika vijiji vya Ntapisi na Bwibuka. Ukanda huu ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao ya mpunga, mahindi, mihogo, maharage, mbaazi, kokoa na matunda mbalimbali. Pia wakulima wa maeneo haya hufuga ng'ombe wa kienyeji (asili), mbuzi, nguruwe nk.

**UKANDA WA KATI:**

Unaundwa na Kata za Lwangwa, Kabula na Sehemu Kata ya Lupata katika vijiji vya Lupata, Mpanda na Nsoso. Ukanda huu kwa sehemu kubwa umefunikwa na mazao ya kudumu kama migomba, kahawa, chai, miwa nk. Pia mazao mbalimbali ya msimu hulimwa katika ukanda huu kama mahindi, maharage, karanga, viazi vitamu, viazi mviringo, mihogo, mbogamboga na matunda mbalimbali.



Wakulima wa maeneo haya hujishughulisha pia na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na wa kienyeji kwa kiasi kidogo, nguruwe, mbuzi wa maziwa nk.

**UKANDA WA JUU:**

Ukanda huu unaundwa na kata za Mpombo, Isange, Kandete na Luteba. Ukanda huu ni maarufu kwa kilimo cha viazi mviringo, mahindi, njegere, mazao ya bustani, na matunda. Wakulima wa maeneo haya pia ni wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, nguruwe, mbuzi, kuku nk. Zana za kilimo zitumikazo katika ukanda huu ni jembe la mkono 97% na matrekta 3%.

**UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI**

Hali ya ukusanyaji wa mapato ya Ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo imeongezeka kutoka asilimia 97 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia asilimia 103.04 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Katika mwaka wa fedha wa 2020/201 makisio kwa mwaka yalikuwa ni kukusanya Tshs. bil. 1,523,020,000.00 lakini zilikusanywa Tshs. bil. 1,483,467,521.54 ambazo ni sawa na asilimia 97. Mwaka 2021/2022 makisio kwa mwaka yalikuwa ni kukusanya Tshs. bil. 1, 593,938,000.00 zikakusanywa Tshs. bil. 1,667,325,646.68 ambazo ni sawa na asilimia 105.

Mwaka 2022/2023 makisio yalikuwa ni kukusanya Tshs. bil. 1,813,245,119.00 lakini zilikusanywa Tshs. bil. 1,868,361,231.65 ambazo ni sawa na asilimia 103.04. Kwa mwaka 2023/2024 makisio yalikuwa ni kukusanya Tshs. bil. 2,000,000,000.00 lakini hadi kufikia mwezi Octoba zilikusanywa Tshs. bil. 1,000,623,402.86 ambazo ni sawa na asilimia 50.03. Jumla kuu ya makisio ni Tshs. bil. 6,930,203,119.00 na makusanyo jumla kuu ni Tshs. bil. 5,655,080,450.01 ambazo ni sawa na asilimia 81.6.


**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI SEKTA YA UTAWALA.**

Katika ukamilishaji wa miundombinu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipokea Tshs. bil. 2 kutoka serikali kuu kwa ajili ukamilishaji wa jengo la Utawala na kwa mwaka 2022/2023 kiasi cha Tshs. mil. 900 zikiwemo Tshs. mil. 750 zilitolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Utawala na kiasi cha Tshs milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji.

Aidha kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 Tshs. mil. 300 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa samani katika jengo la Utawala.

**SEKTA YA AFYA.**

Kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 Halmashauri ilipokea Jumla ya Tshs. bil. 3,595,233,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, kati fedha hizo Tshs. bil. 2,957,733,000.00 zilipokelewa toka Serikali Kuu, Tshs. mil. 500,000,000.00 fedha za TOZO za Miamala za simu, Tshs. mil. 90,000,000.00 fedha za UVICO na Tshs. mil. 47,500,000.00 fedha za mapato ya ndani zilizotumika katika ukamilishaji wa zahanati ya Nsoso.



ANYOSISYE NJOBELO - MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO



LOEMA PETER - MKURUGENZI HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

**ELIMU SEKONDARI**

Kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. bil. 3,424,180,028.00 zikiwa ni fedha kutoka Serikali Kuu, SEQUIP, EP4R na Pochi la Mama kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu.

**ELIMU MSINGI**

Kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024 halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. bil. 1,927,877,980.00 kutoka Serikali Kuu, EP4R na BOOST kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu.

**UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo imekuwa ikiwawezesha wananchi kiuchumi kupitia utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa mchanganuo ufuatao;-

| Mwaka | Kiasi Kilichotengwa | Kiasi Kilichotolewa kwa Vikundi | Idadi ya Vikundi Vilivyonufaika |
|---|---|---|---|
| 2020/2021 | 91,335,870.01 | 361,000,000.00 | 85 |
| 2021/2022 | 100,090,000.00 | 425,500,000.00 | 100 |
| 2022/2023 | 119,367,511.86 | 175,000,000.00 | 20 |
| 2023/2024 | 55,940,000.00 | 0 | 0 |
| JUMLA KUU | 366,733,381.87 | 961,500,000.00 | 205.00 |

# WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA (TEMESA) MKOA WA MBEYA

## “TEMESA MPYA INAYOTOA HUDUMA BORA NA YA KISASA KWA UMMA”

**1.0 UTANGULIZI**

Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) mkoa wa Mbeya ni upo chini ya Wizara ya Ujenzi. TEMESA ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na.30 ya mwaka 1997 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na.254 la tarehe 26 Agosti, 2005, na kuzinduliwa rasmi tarehe 23 Juni, 2006.

TEMESA ilianzishwa kuchukua majukumu ya iliyokuwa Kurugenzi ya Ufundi na Umeme (Electrical & Mechanical Division - E & M) chini ya Wizara ya Ujenzi. Kurugenzi ya Ufundi na Umeme ilianza tangu mwaka 1925 chini ya Kurugenzi ya kazi za Umma (Public Works Department – PWD).

**1.1 DIRA (VISION)**

Dira ya Wakala wa Ufundi na Umeme ni kuwa na Taasisi yenye ufanisi na ubunifu inayotoa huduma za Kihandisi Tanzania kwa ajili ya kumridhisha mteja.

**1.2 DHIMA (MISSION)**

Dhima ya Wakala wa Ufundi na Umeme ni kutoa huduma za uhakika, salama na zenye ubora wa hali ya juu katika fani za uhandisi mitambo, umeme na elektroniki, huduma za vivuko na ukodishaji mitambo kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

**2.0 MAJUKUMU YA WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA (TEMESA)**

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania Mkoa wa Mbeya unatoa huduma zifuatazo kwa kutumia vifaa vya kisaa na wataalamu wabobezi:-**

i. Kufanya ukaguzi, vipimo na matengenezo ya magari, pikipiki, jenereta na Mitambo.

ii. Kufanya ukaguzi, vipimo, usimikaji na matengenezo ya mifumo ya Umeme, Mabarafu, Viyoyozi, taa za barabarani, taa za kuongozea magari na Electroniki.

iii. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Umma katika Nyanja za Uhandisi wa Mitambo, Umeme na Elekroniki;

iv. Kukodisha mitambo ya ujenzi barabara.

**3.0 MAADILI YA MSINGI MAADILIYA MISINGI**

**Wakala utafanya kazi na kujipambanua kwa maadili ya misingi ifuatayo**

i. Uadilifu: Kufanya kazi kwa uaminifu na ukweli kwa wateja na wadau mbalimbali.

ii. Utendaji: Kazi wa pamoj: kufanya kazi kwa pamoja na kwa kushirikiana miongoni na watumishi ili kufikia malengo yaliyo kusudiwa

iii. Utaalamu: Kuhakikisha tunazingatia utaalamu na kufanya kazi kwa weledi wa hali ya juu.

iv. Uwajibikaji: Kujituma katika utendaji kazi na kutimiza matakwa ya wadau na Taifa kwa ujumla.

v. Uwazi: kufanya kazi kwa uwazi na kuwa tayari kukaguliwa katika masuala ya kifedha na kiutendaji.


*Meneja wa TEMESA mkoa wa Mbeya, Mhandisi Clement Abadyame*


*Karakana ya wakala wa ufundi na UmemeTanzania Mkoa wa Mbeya*


*Mtaalamu kutoka kitengo cha uchongaji akichonga “block” ya injini kwa ajili ya kuvisha “sleeve”*


*Maalamu wa kitengo cha ukaguzi (inspection section) akiendelea na kazi ya uchunguzi wa gari kwa kutumia computer mpakato (car diagnostic mashine*



*Moja ya mashine ya ujenzi (heavy duty roller compactor) wa barabara mali ya TAMESA Mkoa wa Mbeya ikiendelea na kazi Wilayani Chunya*


*Mtaalamu kutoka kitengo cha matengenezo ya magari akitoa lingi kwenye taili kwa kutumia mashine maalumu (hydraulic tyre remover)*


*Gari la serikali ikifanyiwa ukaguzi katika karakana ya TEMESA Mkoani Mbeya kwa kutumia mashine ya kisasa (3D alignment mashine) kupima “ wheel alignment”*


*Waziri wa Ujenzi Mh Innocent L. Bashungwa akikagua na kupata maelezo ya mashine ya kisasa ya kufanya “tyre balancing” i.e. computerized tyre balancing mashine*


*Waziri wa Ujenzi Mh Innocent L. Bashungwa akikagua na kupata maelezo ya vitendea kazi vya kisasa TEMESA Mkoa wa Mbeya*


*Maalamu wa kitengo cha upigaji rangi za magari akifanya maandalizi ya awali kuliandaa gari kabla ya kupigwa rangi*


*Picha ya pamoja ya Waziri wa Ujenzi Mh Innocent L. Bashungwa watumishi wa karakana ya TEMESA mkoa wa Mbeya*


*Wataalamu kutoka kitengo cha matengenezo TEMESA Mkoa wa Mbeya wakiendelea na matengenezo ya gari ya mteja*


*Moja wapo ya mitambo ya TEMESA Mbeya ikiendelea na ujenzi wa barabara mkoani Rukwa eneo la MUZE*


*Mtaalamu kutoka kitengo cha ufuaji vyuma (welding & fabrication) akiendelea na kazi ya kutengeneza baadhi ya vifaa vya breki ya kangavuke inayotembea (mobile generator)*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

## MAFANIKIO YA OFISI YA SIDO MKOA WA MBEYA KUPITIA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

# SIDO MBEYA: Tumetengeneza mashine 254 za wajasiliamali kupitia Kituo cha Uendelezaji wa Teknolojia.

**Picha za mashine mpya zilizokabidhiwa kwenye kituo cha uendelezaji wa teknolojia kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita.**



**Press brake machine**



**Press brake machine and shear machine**



**Plasma cutting machine.**

**Na KOKU DAVID-** *MBEYA.*

Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) lilianzishwa kwa sheria ya Bunge ya mwaka 1973 kwa lengo la kupanga, kuratibu, kuendeleza na kutoa huduma mbalimbali kwa viwanda/ biashara ndogo na za kati . Shirika linazo ofisi katika kila mkoa wa Tanzania Bara. Hadi leo SIDO imebaki kuwa mhimili mkuu wa serikali katika kuendeleza viwanda/ biashara ndogo na za kati.

Shirika linatekeleza kazi kuu nne katika kuhudumia wananchi ambazo ni Uendelezaji wa Teknolojia, Mafunzo ya Biashara na Huduma za Ugani, Habari, Masoko na Uwekezaji pamoja na huduma za fedha.

Kwa upande wa Uendelezaji wa Teknolojia, ofisi ina kituo cha Uendelezaji wa Teknolojia kinachohusika na utengenezaji wa mashine zinazoongeza thamani kwenye minyororo mbalimbali ikiwemo mazao ya kilimo, madini, misitu nk.

Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kukipatia kituo mashine za kisasa (semi-automated machine) zenye thamani ya Tshs. milioni 380,000,000 kwa ajili ya utengenezaji wa mashine mbalimbali pamoja na vipuli.

Aidha kwa kipindi hicho kituo kimeweza kutengeza mashine 254 za wajasiriamali kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo nchini na kupelekea upatikanaji wa ajira 762.

Tunamshukuru Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuipatia SIDO Mbeya fedha za kutengeneza miundombinu ya barabara kwenye soko la SIDO Mwanjelwa na hivyo kusaidia kupunguza kero kwa wafanyabiashara hususani nyakati za masika zilizokuwa zinasababisha uharibifu wa maligahfi za wajasiriamali pamoja na njia kutopitika na kufifisha shughuli za uzalishaji.

Kwa sasa miundombinu hiyo inapitika kwa urahisi na kupelekea kuongezeka kwa mapato ya serikali ya mtaa wa viwanda Mwanjelwa.

Katika Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ilipata fedha za mikopo kupitia Wizara ya Viwanda wenye thamani ya Tshs milioni 180 kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali wadogo.

SIDO tumekuwa tukikopesha fedha hizo kupitia mfuko wa wajasiriamali wadogo uitwao - NEDF (National Entrepreneurship Development Fund). Jumla ya ***Tshs. milioni 481*** zilikopeshwa kwa watu 120 na kupelekea ongezeko la ajira 480 kwa vijana.

**Picha za miundombinu ya barabara**











**Picha za mashine mbalimbali zilizotengenezwa na kituo cha uendelezaji wa teknolojia kwa ajili ya wajasiriamali.**



**Illusion Machine for Gold extraction**



**Illusion machine, heater and control box for Gold extraction.**




**Wet Ball mill.**

# TFS MBEYA YAJIVUNIA MAFANIKIO YALIYOTOKANA NA SERIKALI YA AWAMU YA SITA.

## >>The Royal Tour yawezesha ongezeko la watalii hadi kufikia 3,404



Lusibalwamisi



Muonekano wa Mlima Rungwe

**Na KOKU DAVID-**
*Rungwe.*

Katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kuleta maendeleo nchini, kupitia Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mh.Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imefanikiwa kutekeleza Majukumu yaliyopangwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Baaddhi ya mafanikio yaliyofikiwa katika Mkoa wa Mbeya ni:-

- Mkoa wa Mbeya una hifadhi za misitu 30 yenye eneo la hekta 306,669 zinazosimamiwa na TFS. Hali ya uhifadhi wa rasilimali za misitu umeimarika kutokana na upatikanaji wa fedha kwa wakati zinazowezesha kutekeleza shughuli za uhifadhi kama vile doria za mara kwa mara, utoaji wa elimu ya uhifadhi kwa jamii na wadau mbalimbali na kuwezesha matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

- Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, TFS imezalisha jumla ya miche 3,065,736 kupitia bustani zake zilizopo kwenye Ofisi yake ya Kanda na Mashamba ya Miti ya Kawetire na Kiwira. Kati ya miche iliyozalishwa, jumla ya miche 1,757,978 ya aina mbalimbali iligawiwa kwa jamii kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yao kama sehemu ya mchango wa Serikali katika kuhifadhi Mazingira.
- Kuanzishwa kwa Shamba la Nyuki Kipembawe lenye ukubwa wa hekta 20,728 katika wilaya ya Chunya. Uanzishwaji wa shamba la nyuki umelenga kuongeza uzalishaji wa mazao bora ya nyuki yanayokidhi mahitaji ya soko la kitaifa na kimataifa pamoja na kuchangia pato la Taifa. Pia kupitia uwepo wa shamba la nyuki Kipembawe, jamii inanufaika kwa kupatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki, fursa ya ajira na uwekezaji wa shughuli za utalii wa nyuki (Api tourism).
- Kupitia Serikali, TFS imefanikiwa kujenga nyumba ya watumishi (Ranger Post) katika kijiji cha Bitimanyanga ambayo itarahisisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki katika wilaya ya Chunya.
- Kupitia utekelezaji wa shughuli zake za kila siku, TFS katika Mkoa wa Mbeya imetoa ajira zipatazo 70 za mkataba na 1,210 za muda/kutwa kwa jamii.
- Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Utalii ikolojia katika Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe na Kawetire View Point. Vyoo 3 vimejengwa, Kilometa 30 za njia za watalii (Nature Trail) na "view point" 3 zimeendelezwa kwa kuwekewa sehemu za kupumzikia (huts), umeme na maji.

Pia, kupitia fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kukabiliana na madhara ya UVIKO -19, TFS imefanikiwa kujenga njia za watalii na kukarabati barabara kwa urefu wa Km 6 kutoka eneo la Iduda kuelekea Ziwa Ngosi (Tankini Road) ambayo hapo awali ilikuwa haipitiki kiurahisi.

- Kupitia filamu ya "Tanzania The Royal Tour" kumekuwa na ongezeko la idadi ya watalii mpaka kufikia 3,404 katika Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe na Kawetire View Point.

Mipango iliyopo

- TFS inaendelea kuboresha mazingira ya kazi kama vile ujenzi wa ofisi, nyumba za watumishi (ranger posts) na upatikanaji wa vitendea kazi muhimu kama vyombo vya usafiri.
- TFS inaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za kila siku.
- Kwa kuwa filamu ya "Tanzania The Royal Tour" imepelekea kuwepo kwa ongezeko la watalii hadi kufikia 3,404 katika Mkoa wa Mbeya, miundombinu ya utalii inaendelea kuimarishwa ili kuweka mazingira wezeshi kwa shughuli za utalii. Aidha, Uwekezaji wa kutosha unahitajika kwenye maeneo ya vivutio ili shughuli za utalii zifanyike kikamilifu na kuchangia ipasavyo katika Pato la Taifa, hivyo wawekezaji wanakaribishwa.
- TFS inaendelea na jitihada za kubaini vivutio vipya vya utalii vinavyopatikana katika maeneo yake ya usimamizi.
- Utalii wa nyuki kama zao jipya la utalii nchini liendelee kutangazwa ili litumike kuongeza mapato ya Serikali.

### MAENEO YA VIVUTIO VYA UTALII NA FURSA ZA UWEKEZAJI ZINAZOSIMAMIWA NA TFS KATIKA MKOA WA MBEYA

**A: KAWETIRE VIEW POINT:** Ni eneo linalopatikana kwenye shamba la miti Kawetire lenye mandhari nzuri ambapo mtalii awapo hapo ana uwezo wa kuona vizuri bonde la Usangu na ana uwezo wa kuona barabara zipitazo juu ya milima zenye kona ambazo zina mvuto kwa watalii. Lina upepo mwanana na hali ya hewa tulivu. Kuna umbali wa Km 26.2 kutoka Mbeya mjini na linafikika kiurahisi kwa barabara ya Mbeya-Chunya.

**B: HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA MLIMA RUNGWE:** ni miongoni mwa Hifadhi za Mazingira Asilia 23 zinazosimamiwa na TFS. Hifadhi hii inapatikana Mkoani Mbeya katika Wilaya ya Rungwe na Mbeya Vijijini ambayo kwa mara ya kwanza ilipandishwa hadhi mwaka 2009 na ndipo shughuli za utalii zilipoanza rasmi.

Hifadhi hii inajumuisha misitu mitatu ambayo ni Msitu wa mlima Rungwe, Msitu wa Mporoto pamoja na Msitu wa Sawago ambayo kwa pamoja hufanya msitu huo kuwa na ukubwa wa hekta 24,680.5. Aidha, hifadhi inafikika kwa urahisi kutoka uwanja wa ndege wa Songwe pia kwa njia ya barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Mbeya.

Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe ina vivutio vingi vya utalii miongoni mwa vivutio hivyo ni Mlima Rungwe, Ziwa Ngosi, Rungwecebus kipunji, kinyonga mwenye pembe tatu, Craters(Mashimo makubwa yaliyotokana na mlipuko wa volkano) n.k

***Sifa za Vivutio vya Utalii vinavyopatikana kwenye Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe.***

**MLIMA RUNGWE NA SIFA ZAKE.**

1. **Mlima Rungwe:-** Ni mlima mrefu Nyanda za Juu Kusini wenye urefu wa mita 2981 kutoka usawa bahari uliotokana na mlipuko wa volkano.

Pia kuna vivutio vya utalii kama kreta(mashimo makubwa) zilizopatikana baada ya mlipuko ambazo ni Lusiba lukafu na Lusiba Lwamisi.

**SHUGHULI ZA UTALII ZINAZOFANYIKA KATIKA MLIMA RUNGWE.**

- Kutembea ndani ya msitu
- Kupanda mlima,
- Kuweka kambi za kitalii ndani ya hifadhi
- Kuangalia wanyama na ndege,
- Utalii wa picha na Utafiti,
- Utalii wa Michezo (Marathoni/ Forest trail),
- Upigaji picha wa kibiashara,
- Utengenezaji wa Makala (Documentaries).



*Rungwecebus Kipunji*



Kinyonga wa pembe tatu (Uporoto three horned chameleon)

Shughuli hizi ni rafiki kwa mazingira na ndio hutumika kama chanzo cha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali

**ZIWA NGOSI NA SIFA ZAKE.**

**2. Ziwa Ngosi:-** Ziwa hili linapatikana maeneo ya Mbeya vijijini na Rungwe na ni ziwa la pili kwa ukubwa Barani Afrika kati ya maziwa yatokanayo na mlipuko wa volcano. Ziwa hili lina kina chenye urefu wa mita 74, upana wake ni km 1.6 na urefu ni km 2.5.

Muonekano wake unaakisi ramani ya bara la Afrika.

Maji ya ziwa hili hubadilika rangi (kuna wakati huwa na rangi ya bluu, kijani na wakati mwingine nyeusi).

Inasemekana wazee waliamua kulihamisha kutokea mji wa Mwakaleli (Tukuyu) na kulielekezea lilipo sasa kutokana na kwamba ndani ya ziwa hilo kulikuwa na nyoka mkubwa aliyekuwa anakula binadamu pamoja na mifugo yao.

***RUNGWECEBUS KIPUNJI* NA SIFA ZAKE.**

**3.*Rungwecebus Kipunji:*-** Ni aina ya nyani ambaye kwa mara ya kwanza aligundulika katika hifadhi hii mwaka 2003 na shirika lisilo la kiserikali (WCS).

Nyani huyu anatabia kama za binadamu na mara nyingi huwa na aibu.

**4. KINYONGA MWENYE PEMBE TATU**

**Kinyonga wa pembe tatu:-** Kinyonga huyu wa pembe tatu ni kinyonga ambaye ni adimu sana na anapatikana kwenye maeneo ambayo yamejitenga huku Nyanda za juu Kusini.

**VIVUTIO VYA MIMEA NA WANYAMA NA SIFA ZAKE.**

**5.Vivutio vya mimea na wanyama mbalimbali:-** Hifadhi ya Mazingira Asilia Mlima Rungwe ina wanyama mbalimbali kama mamalia zaidi ya 80 (Rungwecebus kipunji).

Pia kuna mimea zaidi ya 460 mfano kama (Mtururunga, mswisa au merianthus holystii, mgomba pori n.k).

Kuna ndege zaidi ya 230 kama Hondohondo au hornbill), samaki zaidi ya 10, Amfibia 36, Reptilia 32 kama *Rungwensis bush viper* na zaidi ya aina 282 za vipepeo.

**6. SIFA NYINGINE.**

Hifadhi hii inasifika kwa kuwa na vyanzo vingi vya maji ambavyo vinahifadhiwa kwani zaidi ya asilimia 49 ya maji yanayotoka Mlimani huelekea Ziwa Nyasa na maji mengine yanatumika na vijiji vya Wilaya ya Rungwe chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Maji ya Wilaya (RUWASA).








Kilele cha mlima Rungwe

# BAADHI YA ALAMA ZA MKOA WA MBEYA



Ziwa Ngosi



Mlima Rungwe



Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya



Kilimo cha Mpunga



Msitu wa Kawetele



Soko la Mwanjelwa



Mnara wa Mwenge wa Uhuru

# UHURU KIJANI

Alhamisi Desemba 7, 2023







MAUA YA HIFADHI YA TAIFA KITULO

Gazeti hili hutolewa na Uhuru Publications Limited, S.L.P. 9221 Dar es Salaam